# SAUTI *ZA* WASHAIRI

***Kwa shule za upili***

**Wandishi**
Jibril Adam. Uledi Brian Rop. Kaka Fred. Okwetso Vincent. Matata Hassan. Fransisca Wambua. Allan Chevukwavi. Duncan Mulu. Momanyi Henry

# SAUTI *ZA* WASHAIRI

**© ELONGO PUBLISHERS 2022**
**Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2022.**

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya waandishi kupitia kwa wakili wao.
Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

**ISBN 9798805937973**

---

**Wahariri**
Kaka Fred
Wadi Sandichi
Brian ULedi
Adam Jibril

# YALIYOMO


**YALIYOMO** ........................................................................... iii

**UTANGULIZI.**.........................................................................iv

**AINA ZA MASHAIRI**........................................................................1

- **Sifa za mashairi**................................................................................1

**MAHITAJI MUHIMU KWA UCHAMBUZI WA MASHAIRI**....3

**1.BAHARI YA MASHAIRI**...............................................................3

- **Bahari kutokana na idadi ya mishororo**........................................3
- **Bahari zinazotokanazo na sura ya vina** ........................................4
- **Bahari zizazotokana na idadi ya vipande katika mshororo.**.......6
- **Bahari zinatokana na kibwagizo na kimalizio.** ............................8
- **Bahari kulingana na mpangilio wa maneno**..................................8
- **Bahari kutokana na idadi ya mizani katika mshororo.**.............11
- **Bahari kulingana na mtindo wa kujibizana** ...............................11
- **Bahari kulingana na ujumbe wa shairi**.......................................11

**2.UHURU/IDHINI/KIBALI/HAKI YA MSHAIRI** .......................12

**3.NAFSINENI NA NAFSINENEWA**..............................................14

**6.LUGHA NATHARI/ TUTUMBI/KAWAIDA/ NYEPESI/ SAHILI/RAHISI** .................................................................................15

**7.UMBO/SURA/ MUUNDO WA SHAIRI** ......................................16

**8 MATUMIZI YA LUGHA NA TAMATHALI ZA USEMI** ..........16

**9.DHAMIRA/LENGO/KUSUDI** ........................................................17

**MASWALI NA MAJIBU YA KCSE** ................................................19

**SAUTI MBALIMBALI ZA WASHAIRI** .........................................51

## UTANGULIZI.

Sauti yoyote ile inaposikika, mtu hupatwa na hisia zitokanazo na wito wa ujumbe katika sauti. Sauti zaweza kuwa za vicheko wakati wa furaha, vilio wakati wa majonzi, lalama wakati wa dhuluma, nasaha wakati ambapo maovu yameshitadi. Baadhi ya sauti ni za kimya kimya wala hazisikiki kwa masikio bali watu huhisi kemi na mwangwi wake moyoni.

Washairi wameteremshiwa uwezo wa kupaza sauti hizi. Na kama ilivyotajwa hapo mbeleni, sauti za washairi zinasikika kutokana na kalamu zao. Kila kalamu zinapomwaga wino, tunapata kufunguliwa kurasa za maisha ya kawaida ya waandishi hawa; maisha ya jamii zao, utamaduni wao, mapito yao, dhiki zao, faraja zao na ndoto zao. Hawaandiki kwa huzuni kwa kutaka kwao bali hayo ndiyo wanayopitia. Na hivyo ndivyo wanavyofanya wanapoandika kwa ajili ya kunasihi na kupumbaza.

Diwani hii imekusanya baadhi ya mashairi ambayo yana ujumbe ajwadi. Kama alivyowahi kutaja marehemu *Sheikh Shabaan bin Robert* kwamba, shairi hubeba maneno mateule yanayoakisi mambo kwa namna yake. Kila msomaji anaposoma mashairi yaliyomo humu atafarijika, atahamasika, atakereka na kughadhabishwa, atachochewa hisia na kuiangalia jamii yake tena na tena.

Mkusanyo huu umeshughulikia masuala yanakumba ulimwengu wa sasa. Washairi wamejikusuru kuyapiga darubini masuala ibuka yanayowazunguka kila uchao. Mada za unyumba zimeshughulikiwa kwa undani. Changamoto zinazowakumba vijana kama vile shinikizo la rika, mapenzi ya dhati pamoja na hila zake, zimezamiwa kwa mapana na marefu. Utamaduni wa Kiafrika ambao umekuwa ukipata changamoto haujawachwa nyuma kamwe katika sauti za washairi. Shairi kama vile *Weusi huu* limeweka bayana madhila ya anayopitia mtu mweusi katika ulimwengu wa mbaguano.

Mbali na hayo, yapo maelezo ya kina yanayochambua na kupambanua istilahi za ushairi mbali na kutoa mifano halisi ili kuwapa wepesi wasomaji wanaojifunza na wanaofunza ushairi. Vile vile, maelezo hayo yanatoa mwangaza kwa yeyote yule anayetafiti bahari ya ushairi. Ni matumaini yangu kuwa msomaji atafaidika pakubwa na kuongeza maarifa na uelewa kuhusu mazingira yake.

*Jibril Adam (Abuu Sanaya)*
*Mombasa Kenya,*

*15/11/ 2022.*

# AINA ZA MASHAIRI

Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum wa maneno kwa njia teule na kwa lugha ya mkato. mashairi ya Kiswahili yameainishwa katika aina mbili ambazo ni;

i) **Mashairi Huru_** Haya ni mashairi yanayotungwa na washairi pasipo kufuata sharia au kanuni za utunzi wa mashairi. Watunzi wa aina hii ya mashairi huitwa wanamapinduzi.

ii) **Mashairi ya Arudhi_** Haya ni mashairi yanayotungwa kwa kuzingatia sharia na kanuni za utunzi wa mashairi. Arudhi ndizo sharia na kanuni za kuzingatiwa. Kanuni hizi ni pamoja na:

   a) Kutumia beti zenye idadi sawa na mishororo.
   b) Kuhakikisha kuwa kuna urari wa mizani katika mshororo. Aghalabu mizani minane ukwapi na minane katika utao.
   c) Kuwa na mishororo yenye idadi sawa ya vipande katika shairi zima.
   d) Shairi kuwa na urari wa vina. Vina viweze kufanana kutoka ubeti moja hadi mwingine.
   e) Shairi kuwa na mistari kifu ambayo yanajenga beti zenye muwala na utoshelezi.

**Sifa za mashairi**

Mashairi yana sifa teule zinazoleta utofauti kati ya fani ya ushairi na fani nyinginezo za lugha. Sifa hizo ni pamoja na:

i) Mashairi kuwa na beti ambazo ni vifungu vya mishororo au mistari.

ii) Mashairi kuwa na mishororo. mshororo ni mstari mmoja katika shairi. Mistari hii kwa pamoja huunda ubeti. Mshororo wa kwanza huitwa mwanzo, wa pili mloto, tatu mleo na wa nne huitwa aidha mkarara, kiitikio au kibwagizo mshororo huo ukiwa unarudiwarudiwa katika kila ubeti au kiishio/kimalizo ukiwa hauridiwi rudiwi katika kila ubeti.

iii) Mashairi kuwa na vipande au migao ambayo ni sehemu ya mshororo husika. Mishororo hugawanyika katika vipande mbalimbali na alama ya kituo au koma hutumika kugawanya vipande katika shairi. Kipande cha kwanza huitwa ukwapi, cha pili utao, tatu mwandamo na cha nne ukingo.

iv) Mashairi kuwa na mizani. Mizani ni silabi zinaunda mishororo katika ubeti. Mashairi ya arudhi aghalabu huwa na mizani minane ukwapi (8a) na minane utao(8b) jumla ya mizani 16.

v) Mashairi yana vina mwishoni mwa kila kipande au mgao. Vina ni mizani ya mwisho katika kila ambayo yanaoana au kuwa na urari. Vina vya kipande cha kwanza huitwa vina vya kati au vya ndani na vya kipande cha pili huitwa vina vya mwisho au vya nje. Ufuatao ni mfano ubeti wenye vina vya kati na mwisho.

_________*ri,* __________*ke,*
_________*ri,* __________*ke*
_________*ri*___________*ke,*
_________*ke,* __________*ri.*

Katika kuanisha mashairi katika ubeti, tunazingatia mishororo mitatu ya kwanza kwa sababu mshororo wa mwisho (kibwagizo au kimalizio) huwa vina tofauti.

vi) Mashairi kuwa na kibwagizo. Kibwagizo ni mshororo wa mwisho katika kila ubeti ambao unarudiwarudiwa. Pia huitwa mkarara au kiitikio.

Ili kuelewa zaidi kuhusu sifa za ushairi tutachambua hizi beti mbili za mshairi.

Kuandika insha bora, lazima uwe makini,
Kwanza zingatia sura, kwa insha namba wani,
Kumbukumbu na shajara, na nyingine jiamini,
Uandike insha bora, wala sio bora insha.

Kuna insha bunilizi, nazo za kiuamilifu,
Andika kijua wazi, ni lazima iwe ndefu,
Mia nne sio kazi, ndiyo maneno faafu,
Uandike insha bora, wala sio bora insha.
***(Uledi Brian Rop, Kenya)***

*Shairi hili lina sifa zifuatazo za kishairi:*
Lina beti mbili
Lina mishororo minne kila ubeti.
Lina vipande viwili katika kila mshororo. Ukwapi na utao.
Lina mizani kumi na sita kila kila mshororo. *8a, 8b = 16*
Shairi hili lina kibwagizo: ‘uandike insha bora, wala sio bora insha.’

Vina vina mpangilio ufuatao

Ubeti wa 1

________*ra*, ______*ni*,
________*ra*, ______*ni*,
________*ra*, ______*ni*,
________*ra*, ______*sha*.

Ubeti wa pili

________*zi*, _______*fu*,
________*zi*, _______*fu*,
________*zi*, _______*fu*,
________*ra*, _______*sha*.

## MAHITAJI MUHIMU KWA UCHAMBUZI WA MASHAIRI

### 1. BAHARI YA MASHAIRI

Bahari ya mashairi ni mtindo ambayo mshairi ametumia kuiwasilisha shairi lake. Mshairi anaweza kuyawasilisha mawazo yake kwa namna mbalimbali. Vifuatavyo ni vigezo vya kuzingatia katika kuainisha mashairi katika bahari mbalimbali.

i) Idadi ya mishororo katika kila ubeti
ii) Idadi ya vipande katika kila mshororo
iii) Mizani katika kila ubeti
iv) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
v) Mpangilio wa maneno katika ubeti na kadhalika.

**Bahari kutokana na idadi ya mishororo**

i) Tathmina_ shairi lenye mshororo mmoja katika kila ubeti.
ii) Tathnia_ shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti.
iii) Tathlitha_ shairi lrnye mishororo mitatu katika kila ubeti.
iv) Tarbia_ shairi lenye mishororo mine katika kila ubeti.
v) Takhmisa_ shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti.
vi) Tasdisa_ shairi lenye mishororo sita katika kila ubeti.
vii) Tasbia_ shairi lenye mishororo saba katika kila ubeti.
viii) Naudia_ shairi lenye mishororo minane katika kila ubeti.

ix) Telemania_ shairi lenye mishororo tisa katika kila ubeti.
x) Ukumi_ shairi lenye mishororo kumi katika kila ubeti.

**Bahari zinazotokanazo na sura ya vina**

i) **Mtiririko_** hili ni shairi ambalo vina vyake vya kati na vya mwisho vinaoana katika shairi zima.

Mtiririko wa kwanza

________*ni*, ________*ni*
________*ni*, ________*ni*
________*ni*, ________*ni*
________*na*, ________*na*.

_________*ni*, ________*ni*,
_________*ni*, ________*ni*,
_________*ni*, ________*ni*,
_________*na*, ________*na*

Mtiririko wa pili

_________*na*, ________*ni*,
_________*na*, ________*ni*,
_________*na*, ________*ni*,
_________*ni*, ________*na*.

_________*na*, ________*ni*,
_________*na*, ________*ni*,
_________*na*, ________*ni*,
_________*ni*, ________*na*.

ii) **Ukara_** hii ni bahari ya shairi lenye vina vya kipande kimoja vinavyofanana ilhali vya kipande kingine vinabadilikabadilika.

Mfano:

________*za*, ________*ra*,
________*za*, ________*ra*,
________*za*, ________*ra*,
________*ra*, ________*za*.

________*za*, ________*ma*,
________*za*, ________*ma*,

_________*za*, _________*ma*,
_________*ra*, _________*za*.

_________*za*, _________*ma*,
_________*za*, _________*ma*,
_________*za*, _________*ma*,
_________*ra*, _________*ma*.

iii) **Ukaraguni_** shairi ambalo vina vyake vinabadilikabadilika kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

__________*ta*, ___________*po*,
__________*ta*, ___________*po*,
__________*ta*, ___________*po*,
__________*po*, ___________*ta*.
___________*zi*, __________*mu*,
___________*zi*, __________*mu*,
___________*zi*, __________*mu*,
___________*po*, __________*ta*.

___________*nga*, _________*mbe*,
___________*nga*, _________*mbe*,
___________*nga*, _________*mbe*,
___________*po*, ___________*ta*.

**Masivina /mapingiti-**shairi ambalo halina urari wowote wa vina mbali na kuhifadhi arudhi zingine za utunzi wa mashairi.

---------------------vi,-----------------------we
---------------------ma,----------------------la
---------------------hu,---------------------zwa
----------------------ji,-----------------------ki

-----------------------ji,-----------------------po
-----------------------mu,---------------------ya
------------------------li,------------------------fe
-------------------------da,---------------------chi

**Bahari zizazotokana na idadi ya vipande katika mshororo.**

i) **Utenzi/utendi_** Tenzi ni tungo ndefu zenye pande moja (ukwapi pekee) na ambayo hueleza kuhusu jambo fulani. Kwa hiyo, mashairi yenye pande moja huitwa utenzi, utendi au tenzi. Mifano ya tenzi katika historia ya mashairi ni: utenzi wa mwanakupona wake Mwanakupona binti Shamu, utenzi wa Tambuka/chou cha herekali wake Athman bin Mwengo, utenzi wa hamziya miongoni wa mingine.

Zifuatazo ni beti sita za mwanzo katika utenzi wa mwanakupona wenye beti Zaidi ya mia moja.

*Negema wangu binti,*
*Mchachefu wasanati,*
*Upulike wasiati,*
*Asa ukazingatiya.*

*Maradhi yamenishika,*
*Hata yametimu mwaka,*
*Sikupata kutamka,*
*Neno lema kukwambiya.*

*Ndoo mbee ujilisi,*
*Na wino wa karatasi,*
*Moyoni nina hadisi,*
*Napenda kusimuliya.*

*Kisake kutakarabu,*
*Bissimillahi kutubu,*
*Umtaye na habibu,*
*Na sahabaze pamoya.*

*Ukisa kulitangaza,*
*Ina la mola muweza,*
*Basi tuombe majaza,*
*Mngu tatuwafikiya.*

*Mwana adamu si kitu,*
*Na ulimwengu si wetu,*
*Walau hakuna mtu,*
*Ambao atasaliya.*

**ii)Mathnawi_** shairi lenye vipande viwili katika kila mshororo; ukwapi na utao.

Mfano

____________,___________,
____________,____________,
_____________,___________,
_____________,___________,

_____________,_____________,
_____________,_____________,
_____________,_____________,
_____________,_____________.

**iii)Gungu** –shairi lenye ukwapi pekee kama utendi ila tofauti hapa ni kuwa kipande kimoja hiki ambacho ndicho kimetengeza mshororo, ni kirefu kwa kila ubeti. Tazama mfano wa gungu.

Ndiwe uliniopoa kwa lindi la umaskini.
Ndiwe ulinikwepua kwa shida za ulimwenguni.
Ndiwe mwana wa kwetu wa kuitwa rafiki jirani.
Ndiwe niyekuita msamaria Bibliani.

**iv)Tumbuizo_** Hili ni Shairi lenye vipande vitatu; ukwapi, utao na mwandamo katika kila mshororo lakini lina mizani minane katika kila kipande.

____*8a*____, ____*8b*_____, ____*8c*____,
____*8a*____, ____*8b*_____, ____*8c*____,
____*8a*____, ____*8b*_____, ____*8c*____,
____*8a*____, ____*8b*_____, ____*8c*____.

**v)Ukawafi_** shairi lenye vipande vitatu visivyo na idadi sawa ya vipande.

____*4a*____, ____*5b*_____, ____*6c*____,
____*4a*____, ____*5b*_____, ____*6c*____,
____*4a*____, ____*5b*_____, ____*6c*____,
____*4a*____, ____*5b*_____, ____*6c*____.

**vi)** **Bantudi**-shairi la vipande vinne kwa kila mshororo yaani utao, ukwapi, mwandamizi na ukingo.

____4a___,_____5b____,____6c____,_____7d_____
____4a___,_____5b_____,___6c____,_____7d_____

**Bahari zinatokana na kibwagizo na kimalizio.**

i) **Msuko_** hii ni bahari ya shairi ambalo vina vya mshororo wa mwisho ni chache. Katika shairi hili, mishororo ya kipande cha kwanza ni mitatu ilhali ya mshororo wa mwisho ni kipande kimoja.

*______8a_____, ____8b______, =16*
*______8a_____, ____8b______, =16*
*______8a_____, ____8b______, =16*
*______8a_____.                    =8*

ii) **Sabilia_** shairi lisilokuwa na kibwagizo kwa hivyo lina kimalizio.

**Bahari kulingana na mpangilio wa maneno**

i) **Kikwamba_** shairi linaloanza kwa neno moja katika mshororo wa kila ubeti.

**1. SIMWANDAMI**

*Simwandami mpumbavu, mwenda tezi na Omoni,*
*Simwandami si mwelevu, marejeleo ngamani.*
*Simwandami makatavu, huyaola maozini,*
*Simwandami angakiri, kuacha kufanya mawi.*

*Simwandami mwacha nyavu, enda kuzama majini,*
*Simwandami si mpevu, kenda kuvuwa na nini?*
*Simwandami mkomavu, sa wamuandamiani?*
*Simwandami angakiri, kuacha kufanya mawi.*

*Simwandami mwenye wivu, simwandami aswilani,*
*Simwandami msikivu, sijelia laitani,*
*Simwandami mwenye kovu, kumbukumbu zi moyoni,*
*Simwandami angakiri, kuacha kufanya mawi.*

*Simwandami mwenye nguvu, kujivuna mtaani,*
*Simwandami nyama ndavu, haziheshimu kanuni,*
*Simwandami zangu mbavu, atazivunja jamani.*
*Simwandami angakiri, kuacha kufanya mawi.*
*(Uledi Bryan_ kinda mtunga nudhuma)*

ii) **Pindu/nyoka/mkufu_** shairi ambalo maneno yake ya ukwapi yanatumika kama maneno ya kuanza katika ukwapi wa mshororo unaofuatia.

Mfano
*Nisemayo kadirini, muyaweke akilini,*
*Muyaweke akilini, yawafae maishani,*
*Yawafae maishani, siku zenu za usoni,*
*Siku zenu za usoni, muishipo duniani.*

*Muishipo duniani, afiya zingatieni,*
*Afia zingatieni, muwe na siha mwilini,*
*Muwe na siha mwilini, maradhi yasiwahini,*
*Maradhi yasiwahini, mfukiwe kaburini.*

*Mfukiwa kaburini, kilo zako ishirini,*
*Kilo za ishirini, kama usufi begani,*
*Kama usufi begani, kukubeba viganjani,*
*Kukubega viganjani, kama mkoba jamani.*
***(Uledi Bryan_ kinda mtunga nudhumu)***

iii) **Zivindo_** shairi lenye sifa kama za kikwamba. Huanza kwa neno moja. Tofauti na kikwamba ni kuwa zivindo hurudia vitawe na kufafanua maana mbalimbali ya vitawe hivyo.

***KAMUSI YA VITAWE.***
*Vua ya awali vua, kutoa nguo mwilini,*
*Vua ya pili epua, samaki toka majini,*
*Vua ya tatu okoa, mtu toka hatarini,*
*Vua hili neno vua, litumie kwa makini.*

*Wamba hela kuadama, huna kitu mfukoni,*

*Wamba kama kwenye ngoma, kufunga nyuzi ngozini,*
*Wamba kuzagaa nyama, iwavyo makaramuni,*
*Wamba kwako nasukuma, uliweke mpangoni.*

*Shuka lilojaza uzi, hutandikwa kitandani,*
*Shuka teremka ngazi, toka juu kwenda chini,*
*Shuka bei kama ndizi, au pungua thamani,*
*Shuka nyingine ni vazi, la kuvaliwa mwilini.*

*Rai ya kwanza ongoa, mbembeleze mwandani,*
*Rai ya kumtilia, ntu kitu mdomoni,*
*Rai maoni kutoa, kuhusu jambo Fulani,*
*Rai kuwa na afia, kwa uwezo wa manani.*

*Kinga zuia madhara, yasikushike mwilini,*
*Kinga jifanyie dawa, ishi poa duniani,*
*Kinga ngumi ya mikora, usingie taabani,*
*Kinga bora kujikinga, tiba gharama jamani.*

*Kama kwanda mfanano, ushabaha wa usoni,*
*Kama kufanana kuno, ni kizuri kama nini,*
*Kama kukisia tano, huna idadi yakini,*
*Kama afadhali hino, Kama kufa utumwani.*

*Kambarau ni kifaa, na pia huitwa kreni,*
*Kambarau yakufaa, lifti pale ofisini,*
*Kambarau ukambaa, ya chombo cha baharini,*
*Kambarau si hadaa, litumie sentensini.*

*Ota mbegu ya mimea, chipua toka ardhini,*
*Ota ndoto kutokea, ulalapo malazini,*
*Ota mbao kuotea, ikaukiapo ndani,*
*Ota jianika pia, motoni au juani.*
*(Uledi bryan- kinda mtunga nudhumu)*

**iv Ruwaza** –shairi hili hupanga maneno kama picha ya kitu Fulani.mf

*sitanyamaza*
*hata nikiambiwa kunyamaza*

*wawe wa kuja na hila kutaka kunimaliza*
*wasije sema ndimi nawabeza*
*sitanyamaza*

**Bahari kutokana na idadi ya mizani katika mshororo.**

i) **Kikai_** hili ni shairi ambalo mizani ya kipande kimoja ni michache kuliko ya kipande cha pili na hujumuisha mizani ya kila mshororo kuwa aghalabu 12 mf --------4-----------,--------8---------

ii) **Tumbuizo _** shairi lenye mizani 24 kwa kila mshororo kila mshororo ukiwa na vipande vitatu.mf --------8---------,------8---------,-----8------

iii) **Msuko** –Shairi la kibwagizo kifupi kushinda urefu wa mishororo mingine.Hii ni kwa sababu ya mizani michache kwa kibwagizo

**Bahari kulingana na mtindo wa kujibizana**

i) **Ngonjera_** shairi la majibizano lenye wahusika wawili au Zaidi katika shairi moja.

ii) **Malumbano_** ni shairi la majibizani ambalo mshairi anatunga shairi zima la kuangazia jambo naye mshairi mwengine anatunga shairi la kujibu mapigo yake.

iii) **Mandhuma_** shairi lenye vipande viwili. Kipande kimoja kinatoa wazo ila kipande cha pili kinatoa jibu la hilo wazo.

**Bahari kulingana na ujumbe wa shairi**

i)Makiwa/taabili-shari la kumsifu mwendazake na kuwafariji wafiwa
ii)Tongoo-shairi linalojikita kwa maudhui ya mapenzi
iii)Msemele/kifunganyama-shairi linalotoa ujumbe kwa kuficha maana ya ndani kijazanda.
iv)Bariza-shairi la sifo kuhusu kiongozi Fulani na uongozi wake
v)Kiambo –hili hueleza madhari ya mahali Fulani na watu wa mahali hapo

## 2. UHURU/IDHINI/KIBALI/HAKI YA MSHAIRI

Uhuru wa mshairi ni ruhusa ambazo mshairi anapewa kutumiwa katika utunzi wa mashairi ili kuweza kutosheleza arudhi za kishairi. Ruhusa hizo ni pamoja na:

**i) Inkisari**

- Huu ni ufupishaji wa silabi katika neno ili kuleta urari wa mizani.

Mfano

*Mamangu alinambia, mwanangu rudi nyumbani,*
*Usipende kukimbia, kutokomea mjini,*
*Nyumbani kunakufaa, utulie akilini,*
*Nyumbani jama nyumbani, hata kama ni pangoni.*
*(uledi bryan_kinda mtunga nudhumu)*

- Katika ubeti wa kwanza mishororo wa kwanza, mshairi ametumia neno alinambia yenye mizani mitano badala ya aliniambia yenye mizani sita.
- Njia nyingine za kufupisha meno ni pamoja na:
- Kuunganisha maneno mawili kuwa moja. Mfano. Mama yangu kuwa mamangu, mwana wangu kuwa mwanangu, mwana wako kuwa mwanao na kadhalika.
- Kudondosha silabi kisha kutumia o rejeshi katika neno Mfano: Aliyekosa kuwa alokosa, walioimba kuwa waloimba, kilinichonishinda kuwa kilonishinda.
- Kudondosha sauti au herufi katika maneno yenye herufi zinazofanana. Kibainishi hutumika kuonesha kuwa herufi imedondoshwa. Mfano: mtaalamu kuwa mta'lamu, taasubi kuwa ta'subi na mtondogoo kuwa mtondogo'

ii) **Mazida/mazda**

- Huu ni uhuru wa kuzidisha idadi ya silabi katika neno ili kuleta urari wa mizani. Zipo njia nyingi za kuongeza silabi katika neno.
- Kuongezea herufi katika neno. Mfano neno sharti yenye mizani miwili kuwa sharuti yenye mizani mitatu.
- Kuongeza herufi hasa katika irabu zinazojirudia. Mfano walimu kuwa waalimu. Karamu kuwa karaamu.

iii) **Tabdila**

- Huu ni uhuru wa kuongeza herufi katika neno pasipo kuongeza idadi ya mizani ili kuleta urari wa vina.

- Mifano ni kama ifuatavyo:

*Mto kuwa muto*
*Sikio kuwa sikiyo*
*Dunia kuwa duniya*
*Chukua kuwa chukuwa*
*Mkulima kuwa mukulima*

**iv) Kuboronga/kufinyanga sarufi**

- Kuboronga sarufi au kufinyanga sarufi ni kubadilisha muundo wa maneno katika sentensi ili kuleta urari wa vina.
- Kwa kawaida, sentensi huanza kwa kiima kisha kiarifu kikafuata. Mfano iwapo kipande kilikuwa 'mtoto analia sana' ukapata sentensi vina vya mwisho ni 'to' itakujuzu ubadili mstari huo kuwa 'sana alilia mtoto'
- Hebu tunagalie ubeti huu wa shairi:

*Jana kuku alitaga, tulipokuwa nyumbani,*
*Kabla ya mama hakuaga, kuelekea sokoni,*
*Punda akachana mbuga, na mzigo mgongoni,*
*Mifugo wote nyumbani, huleta faida nyingi.*
*(Uledi Bryan_kinda mtunga nudhumu)*

- Katika ubeti wa kwanza mshairi ameboronga sarufi kwa kuandika 'jana kuku alitaga' badala ya 'kuku alitaga jana.'
- Ikiwa angefuata sharia za kisarufi angeharibu mpangilia wa vina.

v) **Utohozi_** huu ni uhuru wa kuswahilisha maneno yenye asili ya kigeni. Mshairi anaweza kuswahilisha maneno ya kizungu, kijerumani na kadhalika.

Mfano

*Sorry badala ya sori*
*Either kuwa aidha*
*Byebye kuwa baibai*
*School kuwa skuli*

**vi) Matumizi ya lahaja**

- Lahaja ni matamshi tofauti tofauti ya maneno katika lugha moja.

- Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kama vile kiunguja, kimvita, kiamu, kibajuni, kigwana n.k. mfano:

*Macho kuwa mato*
*Kichwa kuwa kitwa*
*Njia kuwa ndia*
*Njoo kuwa ndoo*
*Mtu kuwa nchu au ntu*
*Thubutu kuwa subutu*

vii)Maneno ya kigeni

Ni idhini ya matumizi ya maneno ya msimbo tofauti mathalan kiingereza au hata lugha za asili kwa ushairi. mfano

Nipe mbawazi **Mulungu**, niweze kuona mbali
Uniondoleye uchungu, unongezeye pia akili
**Nyasaye** wa huko mbingu, naomba nipawe mali
Mwokozi muumba wangu, naomba nipe kibali

Maneno Mulungu na Nyasaye ni ya kigeni na yametumiwa kuleta urari wa mdundo ama rithimu.

## 3. NAFSINENI NA NAFSINENEWA

- Nafsineni ni sauti ya anayezungumza katika shairi pia huitwa nafsi zungumzi. Sharti mtahini atoe sababu ya kuthibitisha kuwa fulani ndiye nafsineni.

*Angalia mfano ufuatao wa ubeti*

*Vijana nawausia, muache mihadarati,*
*Unga yawaharibia, umri wenu wa kati,*
*Baba ninawanenea, kupitia hii hati,*
*Mihadarati ni sumu, inaharibu maisha.*
*(uledi bryan_ kinda mtunga nudhumu)*

*Katika ubeti huu,* ***nafsineni*** *ni baba. Mstari unaithibitisha ni 'baba ninawanenea'*

**ii)Nafsinenewa** ni hadhira lengwa na pia huitwa nafsi zungumziwa. Vijana wanaotumia mihadarati hapa ndio nafsinenewa– 'vijana nawausia'

**4 TONI/LAHANI YA SHAIRI**

Toni ya shairi ni hisia za nafsineni katika shairi. Hisia hizi huletwa na maneno anayotumia mshairi kupitisha ujumbe. Hisia ambazo pasona anaweza kuwa nayo ni: huzuni, furaha, malalamiko, mshangao na kadhalika.

*Ninalia sina hali, nimefiliwa na ndugu,*
*Kutokanana ajali, katika tariki sugu,*
*Sili mwenzenu silali, sinaye tena ndugu,*
*Lala pema ndugu yangu, mola akughofirie.*

Huyu nafsineni anaomboleza kifo cha ndugu yake. Kwa hivyo ni toni ya huzuni.

**5.MISTARI MISHATA NA KIFU**

Mistari mishata ni mistari isiyokamilika kimaana na huhitaji mstari ufuatao ili maanake itokeze wazi.

Mfano

*Napenda kukuambia, kukuambia ya kwamba,*
*Ukitaka kupotea, mihadarati kuramba,*
*Kweli utajiozea, utakosea muumba,*
*Mihadarati ni sumu, huharibu maisha.*
*(uledi bryan_kinda mtunga nudhumu)*

- Mstari wa kwanza hauna maana kamili pasipokuwa na mstari wa pili.

**ii)Mistari kifu**

- Hii ni mistari yenye kujitosheleza kimaana. Mfano ni mstari wa mwisho unaosema ‘mihadarati ni sumu’ huharibu maisha.’

**6.LUGHA NATHARI/ TUTUMBI/KAWAIDA/ NYEPESI/ SAHILI/RAHISI**

- Huku ni kutumia lugha ya kawaida yenye aya kuweza kuandika muhtasari wa alichomaanisha mshairi katika ubeti. Mfano katika ubeti hapo juu:
- Mshairi anapenda kutuambia ya kwamba tukitaka kupotea turambe mihadarati. Anasema licha ya kuoza pia tutakuwa tunamkosea muumba. Anasisitiza kuwa mihadarati ni sumu inayoharibu maisha.

## 7.UMBO/SURA/ MUUNDO WA SHAIRI

- Huu ni mwonekano wa juu wa shairi. Vigezo vifuatavyo huzingatiwa:

a) Idadi ya mishororo katika kila ubeti
b) Idadi ya vipande katika mshororo
c) Mpangilio wa vina katika shairi
d) Idadi ya mizani
e) Uwepo wa anwani
f) Uwepo wa kibwagizo
g) Mpangilio wa maneno
h) Idadi ya beti

## MATUMIZI YA LUGHA NA TAMATHALI ZA USEMI

**Methali:** Methali ni muhtasari wa maneno ambayo hutumiwa na jamii-lugha kuwasilisha itikadi zao. Ni kauli fupi ambazo hutoa ukweli fulani wenye lengo la kuusia, kuonya, kufundisha, kutoa hukumu,

kufahamisha.

**Mifano:**

Chema hakidumu - kitu kizuri hakina maisha marefu.

Ukweli ukidhiri, uongo hujitenga - ukweli una nguvu kuliko uongo. Mifano zaidi ya tamathali ni kama

-tashibihi

-takriri

-tashihisi

-taniaba

-tabaini

-chuku

-tanakali za sauti

-ubalagha

-nahau

-nidaa

-istiari

-tanakuzi
-kweli kinzani
-taswira
-koja

Tanbihi maswli ya mbinu hizi za lugha huambatana na maswali ya muhimu wa mbinu hizo. Inabidi kufahamu kuwa mbinu hizi hutumiwa mara kwa mara kusisitiza ujumbe.

## 9.DHAMIRA/LENGO/KUSUDI

Dhamira ni kusudio linalomsukuma mshairi kuandika shairi.kwa shairi la Uledi kwa mfano dhamira ya mshairi ni kuwatahadharisha vijana dhidi ya mihadarati

## 10.MAUDHUI

Maudhui ni hoja kuu zinazozungukia shairi.kwa kurejelea shairi hilo la mihadarati maudhui ni athari za mihadarati.

## 11.MANDHARI NA UMUHIMU WAKE

Hii ni sehemu ambayo inaonyesha mazingira ambayo shairi limetungiwa. Tazama shairi lifuatalo

*Mke niliyemuoa,mahari nikalipia.*
*leo ananizingua,kwa michoro kabobea.*
*Mwilini amejitia,ya ajabu najutia*
*Mimi ntampa talaka, ana michoro mwilini*

*Kuna michoro ya nyoka,kwenye shingo na makwapani*
*Amechora hata paka,chini hapo kitovuni*
*Uoga umenishika,kulala nalala chini*
*Mimi ntampa talaka,ana michoro mwilini*
(wadi sandichi-uketo wa ushairi uk7)

Ni kweli kubaini kuwa mandhari haya ni ya familia ya mke na mme hususan nyumbani.

***UMUHIMU***

-yanaendeleza maudhui ya utamaduni na usasa
-yanajenga hulka za mkewe mshairi

-yanaonyesha kiini cha migogoro nyumbani mwa mshairi

**12.URUDIAJI**

Kuna urudiaji wa aina tofauti kwa kazi ya ushairi:

-**urudiaji wa sauti-** hii ni sauti yamaneno kadha iliyorudiwa kwa mfano kwa shairi la **michoro mwilini** sauti /m/ imerudiwa kwa maneno **mwilin**i na **mimi.**

**-urudiaji wa silabi-** ni silabi za maneno zilizorudiwa kwa shairi.kwa mfano maneno **kawaida** na **kaida** yana silabi **ka** zilizorudiwa

**-urudiaji wa neno-**ni maneno yanayojirudia kwa mfano neno **mim**i kwa shairi la **michoro mwilini**

**-urudiaji wa mshororo/sentensi/kifungu cha maneno-**wakati mshororo umerudiwa hii pia ni dhna ya usambamba mathalan kwa shairi la kibwagizo ambapo kipokeo kimerudiwarudiwa kwa mfano 'mimi ntampa talaka ana michoro mwilini"

**13. ANWANI/KICHWA CHA SHAIRI**

Anwani ya shairi hutambuliwa kwa njia mbili kuu ikiwa umepewa shairi lisilo anwani. Ikiwa shairi lina kibwagizo (mstari wa mwisho unaojirudia) kichwa cha shairi huwa ni kibwagizo hicho au moja ya kipande kimoja cha kibwagizo.

Ikiwa shairi lina kiishio (mstari wa mwisho usiojirudia,)kichwa cha shairi huwa maudhui makuu kwa shari au kipande cha sentensi kinachopatikana zaidi kwa shairi.Ikiwa shairi la **michoro mwilini** lisingalikuwa na kibwagizo,anwani ingalikuwa TALAKA kwa kuwa hayo ni maudhui makuu.

**1. SHAIRI 'A'.**

*Umekata mti mtima*
*Umeangukia nyumba yako*
*Umeziba mto hasira*
*Nyumba yako sasa mafurikoni*
*Na utahama*
*Watoto Wakukimbia*

*Mbuzi kumkaribia chui*
*Alijigeuza Panya*
*Akalia kulikuwa na pala*
*Kichwani*
*Mchawi kutaka sana kutisha*
*Alijigeuza Simba*
*Akalia na risasi kichwani*

*Jongoo kutaka sana kukimbia*
*Aliomba miguu elfu*
*Akaachwa na nyoka*

*Hadija wapi sasa yatakwenda*
*Bwanako kumpa sumu?*
*Hadija umeshika nyoka kwa mkia*
*Hadija umepitia nyuma ya punda*

**SHAIRI 'B'**

*Piteni jamani, Piteni haraka*
*Nendeni, nendeni huko mwendako*
*Mimi haraka, haraka sina*
*Mzigo wangu, mzigo mzito mno*
*Na chini sitaki kuweka*

*Vijana kwa nini hampiti?*
*Kwa nini mwanicheka kisogo?*
*Mzigo niliobeba haupo.*

*Lakini umenipinda ngongo na*
*Nendako*
*Haya piteni! Piteni haraka! Heei!*

*Mwafikiri mwaniacha nyuma!*
*Njia ya maisha ni moja tu.*
*Huko mwendako ndiko nilikotoka*
*Na nilipofikia wengi wenu*
*Hawatafika.*

*Kula nimekula na sasa mwasema*
*Niko nyuma ya wakati*
*Lakini kama mungepita mbele*
*Na uso wangu kutazama*
*Ningewambia siti miaka*
*Mingi.*

## ***Maswali***

a) Haya ni mashairi ya aina gani? Toa saabu
b) Washairi hawa wawili wanalalamika. Yafafanue malalamishi yao

c) Onyesha jinsi kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili

d) Ni vipi Hadija: -
  (i) Amekata mti mtima?
  (ii) Amepita nyuma ya Punda (al.2)
e) Toa mifano 2 ya uhuru wa mashairi kwa kurejelea mashairi haya

f) Kwa kurejelea shairi '**B**' eleza maana ya: -
  *(i) Mzigo*
  *(ii) Siri*
  *(iii) Kula nimekula*
  (iv) *Niko nyuma ya wakati*

## ***Majibu***

1. a) (i) Mashairi huru *(2X1) ala. 2*

ii) Hayazingatii arudhi za betu, vina, mishororo, mizani na kibwagizo *(2x1) ala. 2*

b) i) SHAIRI A – Anamlalamikia Hadija kwa kumuuwa mumewe kwa kumpa sumu.

ii) SHAIRI B – Anawalalamikia vijana ambao wanamcheka eti amezeeka na kupitwa na wakati Wanamramba Kisogo *(2x2) ala 4*

c) i) Katika SHAIRI 'A' - Hadija alidhani kumuua mewe angepata suluhisho lakini badala yake amejiletea matatizo zaidi. Watu sasa wamemsuta kwa kitendo chake na watoto wanamsumbua.

ii) Katika SHAIRI 'B' – Mshairi anawakejeli vijana ambao wnamramba mzee kisogo bila kujua kwamba hawataki kupita. *(2x2) ala.4*

d)i) Amemuua mumewe – Mti mkuu au kichwa cha nyumba.

ii) Anapata shida za Kujitakia – matatizo yamefurika ngyumbani kama mto (ukupita nyuma ya punda atakutega au kukupiga teke) *(2x2) ala.2*

e) Inkisari – Nendako – Niendako
- Mwendako – Mnakoenda
- Bwanako – Bwna yako

*(1x2) ala.2*

f) <u>Mzigo</u> – uzee/umri<u>. Jiri</u> - Tajriba /Waarifa / Elimu ya maisha.
Kula nimekula - Ameishi miaka mingi
Niko nyuma ya wakati - Amebaki nyuma ne usasa

*(4x1) ala.4*

***2***. *Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwandani.*
*Afya yangu dhahili, mno nataka amani*
*Nawe umenikabili, nenende sipitalini*
*Sisi tokea* ***<u>azali</u>****, twende zetu mizumuni*
*Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?*

*Mababu hawakujali, wajihisipo tabani*
*Tuna dawa za asili, hupati sipitalini*
*Kwa nguvu za kirijali, Mkuyati uamini*
*Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani*
*Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?*

*Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,*
*Dawa yake ni subili, au zongo huanoni*
*Zabadili pia* ***sahali,*** *kwa maradhi yalo ndani*
*Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani*
*Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?*

*Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini*
*Daktari k'ona mwili, tanena kensa tumboni*
*Visu visitiwe makali, tayari kwa pirisheni*
*Ukatwe kama fagili,* ***tumbo nyangwe*** *na maini*
*Nifuateni sipitalini, na dawa ziko nyumbani?*

*Japo maradhi* ***dhalili****, kutenguliwa tegoni*
*Yakifika sipitali, huwa hayana kifani*
*Wambiwa damu kaliti, ndugu msaidieni*
*Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani*
*Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?*

*Mizimu wakupa kweli, Wakueleze undani.*
*Maradhiyo ni ajali, yataka vitu thamani*
*Utete huku wawili, wa manjano na kijani*
*Matunda pia asali, vitu vyae shamoni*
*Nifuateni sipati, na dawa zi langoni?*

***Maswali***

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka
(b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili

(c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitalini
(d) Eleza umbo la shairi hili
(e) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi ?
(f) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye shairi: -
(i) Dhalili –..........................................................................................

(ii) Azali -..........................................................................................

(iii) Sahali -....................................................................................
(iv) Tumbo nyanywe ………………………

***Majibu***

a) – Matibabu ya kiasili | Dawa za asili| dawa za Kisasa.

b) kuonyesha kuwa dawa asili zinafaa kwa matibabu kuliko za Kisasa. Watu wazirejele.
c) Ana matibau ya kiasili
Hosptiali kuna operasheni ya visu.
Kuna dawa za asili zisizopatikana hospitali.
*(4X1) ala 4.*
d) Beti Sita.
- Takhmisa| mishoro mitano.
- Mtiririko – vina bvya ukwapi na utao vinafanana katika beti zote.
- Mathnawi – vipande viwili.
- Mizani ni 8,8
- Lina kiisho – mshoro wa mwisho unarudiwa beti hadi beti katika beti zote. *(6x1) ala.6*

e) kupata idai ya mizani inayotakikana

f. i) Dhalili – Kudharauliwa, nyonge, maskini, dhaifu.
ii)Azali – zamani.
iii)Sahali – Urahisi/ wepesi.
iv)Tumbo nyangwe

3. **WAFULA KABILIANA NA KISU**
*Ee mpwa wangu,*
*Kwetu hakuna muoga,*
*Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,*
*Fahali tulichinja ili uwe mwanamme,*
*Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!*
*Iwapo utatingiza kichwa,*

*Uhamie kwa wasiotahiri.*

*Wanaume wa mbari yetu,*
*Si waoga wa kisu,*
*Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,*
*Wewe ndiye wa kwanza,*
*Iwapo utashindwa,*
*Wasichana wote,*
*Watakucheka,*
*Ubaki msununu,*
*Simama jiwe liwe juu,*
*Ndege zote ziangamie.*

*Simu nimeipokea,*
*Ngariba alilala jikoni,*

*Visu ametia makali,*
*Wewe ndiye wangojewa,*
*Hadharani utasimama,*
*Macho yote yawe kwako,*
*Iwapo haustahimili kisu,*
*Jiuzulu sasa mpwa wangu,*
*Hakika sasa mpwa wangu,*
*Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.*

*Asubuhi ndio hii,*
*Mama mtoto aamushwe,*
*Upweke ni uvundo,*
*Iwapo utatikisa kichwa,*
*Iwapo wewe ni mme,*
*Kabiliana na kisu kikali,*
*Hakika ni kikali!*

*Kweli ni kikali!*
*Wengi wasema ni kikali!*
*Fika huko uone ukali!*
*Mbuzi utapata,*
*Na hata shamba la mahindi,*

*Simama imara,*
*Usiende kwa wasiotahiri*

***Maswali***

(a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha
(b) Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani?

(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume
(d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili
(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili
(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili

(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili?

*(i) Mbari*
*(ii) Msununu*
*(iii) Ngariba*
*(iv) Uvundo*

***Majibu***

(a) - Shairi huru
- Halijazingatia kanunu za utunzi wa mashairi wa kuzingatia arudhi

(b) - Anayeimba ni mjomba
- Anayeimbiwa ni mpwa wake
(c) – Anaambiwa uoga ukimtikia huenda ni wa akina mamaye
- Alichinjiwa fahali ili awe mwanaume
(d) – Chuku – *wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo*
- Takriri – kikali
- Asitiari – upweke ni uvundo
- Tashhisi – uoga ukifikia
(e) - Wakulima – Atapewa shamba la mahindi
- Wafugaji – Atapewa mbuzi
(f) – Tabdila – aamushwe – aamshwe
- Inkisari – Mme – mwanamme
- Kuboronga sarufi – Fahali tulichinja tulichinja fahali
(g)- Mbari Ukoo; kikundi fulani

- Msurruu – Anayenuna
- Ngariba – Mtahirishaji
- Uvundo – Harufu mbaya

## 4. **HATIMA YANGU**

*1. Mke wangu wameshanipoka*
*Ndugu zangu, wamedai ububu*
*Wazazi kuzoea kunigombeza*

*2. Juzi mali lilimbikiza*
*Furaha lilitanda*
*Makanwa yalijaziwa*
*Hoi hoi ikawa desturi*

*3. Kilabu tulikwenda*
*Nyama tulichoma*
*Mahali tulizuru*
*Tuliteremsha!*

*4. Leo mambo yamenigeuka*
*Wao masahibu siwaoni*
*Matumbo yakaninguruma*
*Kama radi ya mvua*

*5. Nyumbani nimebaki pweke*
*Mke amenitoroka*
*Watoto wameparara*
*Skuli kugharamia*
*Imegeuka balaa belua*

*6. Ndipo nimeamua*
*Afadhali kitanzi badala ya balaa*
*Kumbe kupanga ndiyo maana*
*Maisha na waasia*

***Maswali:***

(a) Eleza mambo muhimu yanayoelezwa katika shairi hili

(b) Fafanua sifa mbili za anayezungumza katika shairi

(c) Dondoa na ufafanue mbinu zozote mbili za lugha katika shairi hili

(d) Eleza maana ya: -
(i) Ndugu zangu wamedai ububu
(ii) Kumbe kupanga ndiyo maana

**Majibu**

a) (i) Amenyang'anywa mkewe
(ii) Wazazi wake wanamgombeza
(iii) Alipokuwa na mali marafiki walikuwa wengi. Alikuwa akiwapeleka marafiki klabu na walifurahia pamoja wakichoma nyama.
(iv) Mqwandishi hawaoni tena marafiki wote; wameshatoroka. Ana njaa na matatizo mengi sana.
(v) Amebaki pweke, mke ametoroka na watoto wameparara. Mwandishi hawezi kulipa karo.
Sasa ameamua kujitia kitanzi *(4x1= al.4)*

(b) (i) Mbadhirifu –a alitumia mali vibaya
(ii) Mpweke – Ndugu hawamsemezi anaishi upweke
(iii) Mpenda anasa =- Alikuwa akinywa pombe na kukaa sana klabuni *(al. 2 x 3= 6)*

(c) (i) Msemo – Balaa belua
(ii) Jazanda – "Juzi" ni wakati uliopita ilhali 'leo" ni sasa au wakati huu
(iii) Tashbihi – kama radi ya mvua *(2 x 3= al. 6)*

(d) (i) Ndugu zangu wamedai ubub – Ndugu zangu wamekataa kusema nami yaani hawanisemezi kwa hali yangu mpya.
(ii) Kumbe kupanga ndiyo maana- Amegundua kuwa angepanga maisha yake tangu awali atumie vizuri raslimali alizokuwa nazo badala ya kuzifuja *(2x1= al.2)*

5. *1. Nitampa nani, sauti yangu ya dhati*

*Kwa kipimo gani, ingawa kiwakatiti*
*Amefanya nini, la kutetea umati*
*Kipimo ni kipi?*

*2. Yupi wa maani, asosita katikati*
*Alo na maoni, yasojua gatigati*
*Atazame chini, kwa kile ule wakati*
*Kipimo ni kipi?*

*3. Alo mzalendo, atambuaye shuruti*
*Asiye mafundo, asojua mangiriti*
*Anoshika pendo, hata katika mauti*
*Kipimo ni kipi?*

*4. Kipimo ni kipi, changu mimi kudhibiti*
*Utu uko wapi, ni wapi unapoketi*
*Nje kwa mkwapi, au ndani kwa buheti*
*Kipimo ni kipi?*

***Maswali***

a) Eleza umbo la shairi hili
b) Taja na ueleze jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wa ushairi

c) Eleza ujumbe unaowasilishwa na mshairi
d) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha ya nathari
e) Taja bahari **tatu** zinazojitokeza katika shairi na utoe sababu

f) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi hili

*i) Katiti*
*ii) Gatigati*
*iii) Mangiriti*

***Majibu:***

a) Beti nne

- Mishororo mine katika kila ubet (tarbia)
- Mshororo wa nne mfupi (msuko)

- Mizani 6:8 mshororo wa 1-3 kikai
6 mshororo wa mwisho

b) Inkisari – Anoshika
- Alo
- Asosita

Lafudhi – Katiti
- mangiriti

Kutaja 2 mifano 1

c) - Anataka asikike (mawazo yake yasikika)
- Anatafuta atakayoeleza ujumbe wake
- anashindwa atatumia kipimo kipi
- Mtu huyo lazima awe mzalendo aliye jasiri
- Lazima awe anayetambua utu

d) Lugha ya natahria; Aliye mzalendo na alambuaye haya mtu asiye mwoga, aliyejawa na upendo hata wakati wa hatari, Ni kipimo kipi cha kumtambua mtu kama huyu

e) tarbia – Mishororo mine kila ubeti Kikai – Mizani isiyozidi 15
Msuko – Kibwagizo kifupi

f) i) Katili – Kidogo
ii) Gati gati – Ubaguzi
iii) Mangiriti - mambo ya upipi

6. **KIPI NIKITENDE?**

**.** *Tayari ni sarakani, niambie yote johara,*
*Mosi nimpe shukrani, kanizaa bira zira,*
*Wapo haiko hisani, ningefaa kwa uparara***,**
*Kipi takachokitenda, ni nene heko kwa mama?*

**.** *Miezi tisa tumboni, yote nina kajinyima,*
*Kanikopa uchunguni, safari ndefu kazima'*
*Kama kinda kiotani, kiniasa huyu mama'*
*Kipi takachokitenda, ninene heko mama?*

**.** *Baba siku jana madadi,* ***kawa vingaito mambo,***
*Kaolewa na asadi, kachalazwa kwa* ***wimbombo****,*
*Kaona – bali jadili, kuchao puani bombo,*
*Kipi takachokitenda, ninene heko mama?*

**.** *Kila kuchao zarani, kupalilia kondeni,*
*Kachanika mpinini, chungu povuka motoni,*
*Kaviyariya fingani, kinijali jikoni,*
*Kipi tukachokitenda, ninene heko mama?*

**.** *Wa siku hizi vijana, wakahujuru nyumbani,*
*Wengine wao jagina, kawa lofa mutaani,*
*Hali ukashiba nina, afikapo tu, "****kongoni!"***
*Kipi takachokitenda, ninene heko mama?*

**.** *Nawe bwana siwe maya, vita hasha kiwa kombo,*
*Tena simfanye yaya, ya kikoa ndio mambo,*
*Simtende ya hizaya, siwe mwao kila jambo,*
*Kipi takachokitenda, ninene heko mama?*

*. Sasa jamvi nakuja, kisa nimesakarika,*
*Naomba niliyotaja, tatia manani kaka,*
*Nenayo yasiwe ngoja, ili nipokee baraka,*
*Mema nitamtendea, apate futahi pia.*

***Maswali***

(a) Eleza umbo la shairi hili
(b) Kwa nini msanii amshukuru mamaye?
(c) Ni kina nani wanaokashifiwa na msanii? Kwa nini?

(d) Onyesha tofauti katika ujumbe iliyoko katika beti nne za kwanza na mbili zinazofuata
(e) Toa majina mengine yenye maana sawa na haya yaliyotumiwa katika shairi hili:

*(i) Mama*
*(ii) Dawati*
*(iii) Imara/thabiti*

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika kaika shairi:

*(i) Kawa vangaito mambo*
*(ii) Wimbombo*
*(iii) Kongoni*

**Majibu**

a)

3. Beti saba
4. Tarbia – mishororo mine
5. Vina vya ndani na vya nje hubadilika badilika
6. Pande mbili – ukwapi na utao
7. Mizani 8, 8 jumla 16 katika kila mshororo
8. Kibwagizo kipo – kipi titakachotenda, ninene huko mama

b)
Kwa kumza bila zira (chuki)
Kumpenda na kutomuua
Kujinyima yote mazuri kwa niaba yake
Kumtunza mfano wa ndege na makinda wake
Kumtafutia riziki – kufanya kazi (kulima) ili asitaabike
Kumjali
Kutojali visiki katika ulezi wake kama vile baba yake mkali*Zozote 5x1=5*
c)

1. Vijana ambao baada ya kulelewa na kunenepa hawajali wazazi wao (*mama zao*)
2. Akina baba wanaowapiga wake wao kwa makosa madogo madogo
3. Pia akina baba wanaowatesa wake wao. Huwafanya yay nyumabni mwao *Zozote 2x1=2*

d) katika beti nne za kwanza mshairi anaangazia mema aliyotendewa na mama yake ilihali
katika beti mbili zinazofuata anawakashifu wanaowatendea akina mama wao mabaya *Alama 3*

e) Mama – nina (Ubeti wa 2)
Dawati – saraka (Ubeti wa 1)

Imara/ thabiti – jahidi (ubeti wa 3)

f) i) Mambo yakavurugika
ii) Wimbombo – Kipande cha miti cha kupekecha moto. Chuma cha kupuliziz moto
iii) Kongoni – Jina la kumkaribisha mtu

7. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**
**<u>MWANAMKE</u>**
*1. Namwona yu shambani,*
*Na jembe mkononi,*
*Analima,*
*Mwanamama,*
*Mavuno si yake,*
*Ni ya mume wake.*

*2. Namwona viwandani,*
*Pia maofisini,*
*Yu kazini,*
*Hamkani,*
*Anabaguliwa,*
*Na anaonewa.*

*3. Namwona yu nyumbnai,*
*Mpishi wa jikoni,*
*Yaya yeye,*
*Dobi yeye,*
*Hakuna malipo,*
*Likizo haipo.*

*4. Namwona kitandani,*
*Yu uchi <u>maungoni.</u>*
*Ni mrembo*
*Kama chombo,*
*Chenye ushawishi,*
*<u>Mzima utashi.</u>*

*5. Namwona mkekani,*

*Yuwamo uzazini,*
*Apumua,*
*Augua,*
*Kilio cha kite,*
*Cha mpiga pute.*

*6. Kwa nini mwanamke,*
*Ni yeye peke yake,*
*Heshimaye,*
*Haki anakosa,*
*Kwa kweli ni kosa*
***(Muhammed Seif Khatib)***

## ***Maswali***

(a) "**Shairi hili ni la kukatisha tamaa**". Fafanua dai hili kwa kutoa mifano **minne**
(b) Eleza umbo la shairi hili
(c) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari
(d) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima utoe mifano **miwili** ya jinsi ilivyotumika
(e) Onyesha mifano miwili ya ubabadume inayojitokeza katika shairi hili

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi:
    (i) mzima utashi
    (ii) maungoni

## ***Majibu***

a) Linakatisha tamaa kwa sababu

1. Mwanamke anapolima, hafaidiki na mavuno bali yote huchukuliwa na bwanake
2. Mwanamke hubaguliwa na kuonewa ofisini
3. Mahali pake ni jikoni, ujakazi n.k lakini halipwi na tena hapewi likizo (hapumziki)
4. Hutumiwa kama chombo cha mapenzi kukidhia uchuu wa mwanamke
5. Hamna anayemheshimiwa kwa chochote eti kwa sababu ni mke *Zozote 4 X 1 = 4*

b) UMBO

i. Beti sita
ii. Mishororo sita kwa kila ubeti
iii. Vina vya wisho vya mishororo ya kwanza miwili (mwanzo na mloto) ni –ni- isipokuwa ubeti wa sita (mwisho)
iv. Kila ubeti hususan wa kwanza hadi wa tano umeanza kwa neno Nomwona isipokuwa ubeti wa sita – kupelekea shairi hili kuwa kikwamba
*v.* Kila ubeti una kituo tofauti

*Zozote 5X1= 5*

c) Lugha Nathari

Mwanamke hushinda katika boma akipika, akilea, na hata kufua nguo. Licha ya hayo halipwi na tena hapewi nafasi ya kupumzika Tuza

4. Tathmini matumizi ya lugha nathari

d) Tamathali iliyotawala

i) Taswira – hali ya kumwona mke nyumbani na kwingineko katika shughuli mbalimbali

k.m - akiwa nyumbani akipika
- akiwa kitandani uchi
- akiwa mkekani katika utungu wa kujifungua n.k.

*Kutuza: Kutaja mbinu 1 Mifano 2X1= 2 Jumla*
3

e) Mifano ya taasubi ya kiume

i. Katika ubeti wa kwanza, mume anayachukua mavuno kutoka kwa mkewe
ii. Wanaume katika ubeti wa pili wna ubaguzi na kuonea wanawake

f) Msamiati-Mzima utashi

i) Mwenye udiu/ tama kubwa Maungoni
ii. maumbo, viungo vya mwili vinaonekana wazi

## 8. **<u>KIACHE KINACHONG’AA</u>**

*Katu siwe na harara, wala moyo kukupapa,*
*Usichukue hasira, na moyo kutapa-tapa,*
*Utaharibu na sura, mwishowe uende kapa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Mbeleye kina madhara, kile kinachokukukwepa,*
*Mbele yake ni hasara, si chema kitakutupa,*
*Hutaipata ijara, kuchuma ama kukopa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Hicho jangwa la Sahara, si mnofu ni mfupa,*
*Hakina njema ishara, humtupa mwenye pupa,*
*Kibovu kama tambara, hupasuka kama chupa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Kitaleta ufukura, si huko wala si hapa,*
*Kina mengi mazingira, na mbele kitakuchapa,*
*Sijitie usogora, ukavimbisha mishipa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Si kazi yenye ujira, mshahara kukulipa,*
*Ya cheo chenye kinara, na heshima wakikupa,*
*Mbele haina imara, japo leo wajitapa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Japo kazi ya biashara, kutwa wauza makopa,*
*Uwe mtu na kipara, Mwananchi ama Yuripa,*
*Bora uwe na busara, fedha tajaza mapipa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Usione kinang'ara, huku chapiga marapa,*
*Ukimbilie kupora, moyo wako kukuzipa,*
*Kitakugeuza chura, mbele yake utaapa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Usitupe sarara, nyuma kisogo kuipa,*
*Ukaenda kwa papara, kiumbe mbele kitanepa,*
*Kwanza tumia fikira, uchague njema chapa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Na sisemi masihara, hakika kweli nawapa*
*Mlio pwani na bara, wa Mufindi na wa lupa*
*Maneno haya kitara, muarifu na Wachepa,*

*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

*Tamati niliyochora, ya shikeni si kuepa*
*Kisha muwe na basira, na Mola kumuogopa,*
*Kinachokwepa si nyara, ufunge ndani ya kwapa,*
*Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara*

## ***Maswali***

(a) Eleza hii ni bahari gani ya shairi (b) Eleza dhamira ya mshairi (c) Fafanua hasara nne zinazoletwa na tamaa - vile ving'aavyo

(d) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi

(e) Andika ubeti wa tano katika lugha ya nathari

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi

(i) Kuchuma
(ii) Kisogo kuipa

## ***Majibu***

(a) - Pindu, kipande cha kiitikio ndicho kianzio cha ubeti unaofuata
- Tarbia, mishororo minne minne kila ubeti
- Mtiririko, Vina, vya pande zote vinakeketa- tangia ubeti wa kwanza hadi mwisho (yoyote al. 2)

(b) – Kile ulichojaribu kukifanya hakiwezekani usilazimishe, labda ni mapenz ya Mola.
- Si vyote ving'aavyo ni vyema, kabla ya kufanya jambo, fikiria/ tumia busara (2x2=al.4)

(c) – Kuharibika sura
- Humtupa mwenye pupa
- Mbeleni utachapwa
- Huleta hasara
-Kitakugeuza kuwa kitu kingine kisicho na utu *(zozote 4x1=al. 4)*

(d) – Istiari – jangwa la Sahara
- Semi – Kuvimbisha mifupa, kukipa kisogo *2x2=al. 2)]*

(e) Hata ukilipwa mshahara mnono na cheo kikubwa ikiwa mbele kuna majuto kwa sababu
ya majitapo yako, hutafaidi chochote kwa vile mbele utapata madhara *(4x1=al. 4)*

(f) (i) Kuchuma – kupata
(ii) Kisogo kuipa – Kuikataa/kuiacha *(1x2=al. 2)*

*9. Alipokwenda kwao, mamaye alimwambia,*
*Nipa fedha au nguo, nataka kwenda tumia!*
*Nikosapo hivi leo, nipa kisu tajitia!*
*Huzunguka akilia kwa maana ya uketo*

*Ndipo mamaye kawaza, pamwe na kuzingatia,*
*Fedha zako umesoza, na leo zimekwisha,*
*Kisu sikukukataza, twaa upate jitia!*
*Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!*

*Ulipogeuka nondo, nguo ukazingilia,*
*Kakaka kwa vishindo, usisaze hata moya,*
*Leo wanuka uvundo, wambeja wakukimbia!*
*Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!*

*Ukijigeuza nyama, kama Simba ukilia,*
*Watumwa ukawaegema, ukawla wote pia,*
*Pasi kuona huruma, kutoa wahurumia,*
*Mbona hukuzingatia? Wende na ukiwa wako!*

*Si mimi naliokupa,* ***<u>ukata</u>*** *huo, sikia!*
*Kwamba utakuja hapa, nipate kuondolea,*
*Naapa thama, naapa, sina la kukutendea!*
*Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!*

*Tamati, nalikomile, ni hayo nalokwambia,*
*Hapahitaji kelele na kujirisha mabaya,*
*Na kwamba yakutukie, sema yapate n'elea!*
*Zidi radhi kuniwea! Wende na ukiwa wako!*

**<u>Maswali</u>**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (b) Ni maudhui gani yanayojitokeza katika shairi hili

(c) Taja na ueleze tabia za mnenewa katika shairi hili

(d) Mshairi ametumia uhuru wa utunzi. Taja sehemu mbili alikotumia uhuru huo

(e) Eleza umbo la shairi hili

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi: -

(i) Uketo
(ii) Ukata

***Majibu***

(a) Uketo/uhitaji/ukata/ufukara/umaskini (2x1=al. 2)

(b) – Umaskini
- Upweke
- Uwezo
- Uozo wa jamii
- Utovu wa nidhamu
- Ukatili/udhalimu *(zozote 4x1= al.4)*

(c) – Mbadhirifu
- Mwasherati
- Mlalamishi
- Kitatange
- Asiyesikia makanyo
- Mkata
- Mtovu wa heshima *(Kutaja -1, kueleza -1 = al. 2) (2x2=al. 4)*

(d) – Kufupisha maneno (inkisari) nikosapo, nondokea
- Ritifaa k.m n’eelea
- Tashbihi k.m. Kama simba
- Tanakali za sauti k.m. kkka
- Sitiari k.m. ulipogeuka nondo *(1x4=al. 4)*

(e) - Beti sita
Mishororo minne minne
Mizani nane nane
Vipande viwili viwili

Mtiririko wa vina vya mwisho, vya kati vikibadilika badilika Kipokeo *(1x4=al. 4)*

(f) (i) Umaskini

(ii) Umaskini *(1x2=al. 2)*

10 . ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

*Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,*
*Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,*
*Husuda wameikata, hata hawasengenyani,*
*Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja*

*Mchwa nao nikaona, wamejenga masikani,*
*Wafanya bidii sana, uvivu hawatamani,*
*Wao husaidiana, tena hawadanganyani,*
*Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja*

*Nalo jeshi la siafu, hutandawaa njiani,*
*Laenda bila ya hofu, maana ajiamini,*
*Silaha zao dhaifu, meno, tena hawaoni*
*Wa kuwatadia nini? Kwani wanao umoja.*

*Nao chungu wachukuzi, nyama warima njiani,*
*Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani,*
*Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,*
*Katu hawafarakani, wanadamu kwa umoja.*

*Sisi ni wana Adamu, mbona hatusikizani,*
*Tusitietie hamu, ukubwa kuutamani,*
*Wachache wataalamu, tuwasadi kwa imani,*
*Hii "Huyu awezani," yatuvunjia umoja*

***Maswali***

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka.
(b) Ni sifa zipi nne zinazopewa wanaozungumza.
(c) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili.

(d) Eleza muundo wa shairi hili.
(e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari.

(f) Taja mafunzo mawili unayopata kutokana na wahusika wanaozungumziwa.
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hilo.

(i) Chungu
(ii) Tuwasadi

**_Majibu_**

(a) Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
(i) Umoja
(ii) ushirikiano(*yoyote moja = al. 2)*

(b) (i) Nyuki wanafanya kazi kwa umoja- Hawasengenyani
(ii) Mchwa wana bidii/ hawana uvivu
Mchwa husaidiana na hawadanganyani
(iii) Chungu hawafarakani
(iv) Siafu hujiamini (*zozte nne; 4x1=al.4)*

(c) (i) Kubanaga sarufi/ kubananga lugha mfano: -
- Uvivu hawatamani – hawatamani uvivu
- Ukubwa kuutamani – kutamani ukubwa

(ii) Inkisari/ufupisho wa maneno
mf. awezani – anaweza nini
*kutaja alama 1; mfano alama 1 = ala. 2)*

(d) tarbia/nne – mishororo minne katika kila ubeti
Ukaraguni – vina vinavyotofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine

- Kiishio ambacho hakifanani kutoka ubeti hadi ubeti
- Liona beti tano
- Ni la mathnawi – vipande viwili, ukwapi na utao
- Mizani 16 katika kila mchororo, 8,8, (al. 4)

(e) Mwandishi wa shairi anauliza kwa nini sisi ni wanadamu lakini hatusikizani. Huwa tunatamani ukubwa kwa hamu. Hata wale wachache ambao ni wataalamu hatuwaamini. Huwa tunasema kwamba hawawezi chochote. Mshairi anamalizia kwa kusema kwamaba dharau itatuvunjia umoja
*(Tathmini majibu ya mwanafunzi al. 4)*

(f) – Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu
- Bidii ni ushirikiano kazini
- Kujiamini katika yale tuyatendayo maishani *(zozote 2x1= ala. 2)*

(g) (i) Chungu – Wadudu wadogo weusi watambao
(ii) Tuwasadi – tuwasadiki, tuwaamini, tuwakubali.

11. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

*1. Twamshukuru Mwenyezi, Kamwe wingi ukarimu*
*Alo na kiti cha enzi, Mola wetu akramu*
*Kutupa kitu azizi, lugha kutakalamu*
*Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia*

*2. Lugha mkuu mlezi, aleaye binadamu*
*Hata wanyama ja mbuzi, wema lugha wafahamu*
*Hafuguwa simulizi, izaayo tabasamu*
*Lugha huwa ni imamu, ujuwapo kutumia*

*3. Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu*
*Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasama*
*Ikazidisha mapenzi, wapendanao kudumu*
*Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia*

*4. Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu*
*Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu*
*Aidha hufanya kazi, ikawa mustakumu*
*Lugha kwayo ni timamu, ujuwapo kutumia*

*5. Lugha ni mpelelezi, maovu kuwakasimu*
*Huwatowa palo wazi, kashuhudia kaumu*
*Yasifiwa na wajuzi, kuwa ni kitu adhimu*
*Lugha mkuu hakimu, ujuwapo kutumia*

*6. Lugha huizuwa kazi, kutatiza mahakimu*
*Huwaacha kanwa wazi, wakili kitakalamu*
*Muhalifu na jambazi, wakaishinda hukumu*
*Urongo huwa timamu, ujuwapo kutumia*

*7. Lugha iwe ni kiongozi, Kizungu au Kiamu*
*Iwekapo waziwazi, silabi na tarakimu*
*Huyakimu maongezi, yakasikizwa kwa hamu*

*Lugha huwa ni muhimu, ujuwapo kutumia.*

8. *Lugha ni mapinduzi, wanyonge na wajukumu*
*Kadhalika ni jahazi, ya nahodha muhitimu*
*Kufa maji haiwezi, si vina si miizamu*
*Lugha maji zam-zamu, ujuwapo kutumia*

***Maswali.***

1) Eleza maudhui ya shairi hili
2) Eleza muundo wa shairi hili
3) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nadhari/ nadharia

4) Taja huku ukitoa mifano, mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi kuwasilisha ujumbe
5) Eleza maana ya msamiati kama ulivyotumika

i. Azizi
ii. Uhasimu
iii. Adimu.

***Majibu***

(a) Umuhimu wa lugha:

- Lugha nikitu (azizi) cha muhimu
- Lugha hufungua simulizi na kuleta anwani
- Lugha hukuza mapenzi
- N timamu katika nyanja mbalimbali za kazi - Huokoa katika kesi
- Huvuta usikilizaji ikitumiwa vizuri *(zozote 5x1=al.5)*

(b) Mishororoinne kila ubeti – tarbia
imegawika katika vipande viwili – mathinawi
- Mizani ni 16 kila mshoro/ukwapi 8, utao 8
- Vina zi, mu
zi, mu
zi-mu
mu-a
-ukara vya mwisho vinatiririka
- beti ni 8
- Kituo – ukwapi – nitofauti

Kibwagizo – utao – una keketo (*Bahari*)
(c) Lugha hufanya kazi ngumu kama mpagazi. Isitoshe hutumiwa kupana ya siku za usoni/zijazo bila kudhulumu. Hufana mambo yakanyooka nakwa hivyo ni nzuri unapofahamu na kwa hivyo ni nzuri unapoifahamu

(d) Jazanda – Lugha mkuu mlezi – ni mpelekezi
- Lugha ni imamu – ni hakimu mkuu
Mashairi - Lugha hodari mkwezi – ni jahazi -
Huyeyusha sumu – maji zamu - Ndiye mpagazi – zamu
Tashibihi – hata wanyama ja mbuzi
Misemo – huzifyeka pingamizi, huwaaxcha mkamwe
Tashhisi – Izaayo tabasamu
Tabaini – Si vina ci milizamu (zozot 3 = *1x3=al.3)*

(e) Azizi – kitu cha thamani
Uhasimu – Uadui, uhasama, hali ya kufarakana

Adimu – Tukufu/ushujaa/jasiri (al. 3)

12. ***Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali: -***

**SHAIRI A:**

*Tunda la elimu zote, wasema wanazuoni,*
*Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani.*
*Ndipo hadhi aipate, akumbukwe duniani.*

*Elimu bila ukweli, haizidi asilani*
*Giza na nuru muhali, katu havitengamani,*
*Uwongo uje kwa ukweli, itue nuru moyoni.*

*Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani,*
*Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni,*
*Elimu njema miali, iangazayo gizani.*

*Mtu hachomwi na mwiba, na viatu mguuni,*

*Ulimwengu una miiba, tele tele majiani,*
*Elimu ukiishiba, U salama duniani.*

*Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini,*
*Hai ndio waulama, wapaao maangani,*
*Elimu jambo adhima, aso nayo maskini*

*Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni*
*Pale uitafutapo, ujira usitamani*
*Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.*

*Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni,*
*Wao wameongolewa, na ni taa duniani.*
*Kweli wanapojua, watoe bila kuhini.*

*Elimu bila amali, mti usio majani,*
*Haumtii kivuli, aukaliaye chini,*
*Inakuwa mushkeli, wa kushuri insani,*

**SHAIRI B**
*Inakera moyo*
*Hii anga ambayo*
*Huwasonya njiani*
*Watokao mashambani*
*Wa kusalimu kwa bashasha*
*Wanaoshinda kivulini.*

*Chini ya mwembe*
*Wa umma.*

*Inakera moyo*
*Hii sebule ambayo*
*Huwahini mezani*
*Wagotao nyundo kutwa*
*Wa kukabili chakula*
*Wanastarehe daima*

*Chini ya paa*

*La umma.*

## ***Maswali***

(a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa kila shairi la A na B

(b) Haya mashairi ni ya aina gani?
(c) Taja sifa zozote **tatu** za kishairi katika shairi B
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa: -
(i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa saba katika shairi la A
(ii) Katika ubeti wa nne wa shairi la B
(e) Fafanua kwa mukhtasari maudhui ya mashairi yote mawili

(f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha nathari

(g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A
(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi: -

(i) Maulama
(ii) Wameongolewa
(iii) Wagotao
iii) Huwahini

## ***Majibu***

| SHAIRI LA A | SHAIRI LA B |
|---|---|
| **a) Elimu/ elimu ni muhimu** | Kero moyoni (alama 2) |
| **b) Tathlitha/ utatu/ ukara** | Shairi huru (alama 2) |
| **c)- Lina beti nne**<br>**- Idadi ya mishororo hutofautiana katika kila ubeti**<br>**- Hakuna urari wa vina**<br>**- Hakuna kibwagizo**<br>**- Hakuna migao** | |

| **Hoja 3 = alama 3** | |
|---|---|
| **d) i) Tashhisi/ uhaishaji** | ii) Istiara (chini ya paa la umma) yaani starehe alizonazo mwenye mali zinazotokana na jasho la wahitaji |
| **e) Maudhui- umuhimu wa elimu sulubu hawaheshimiwa** | Dhuluma dhidi ya wafanyakazi za sulubu k.m. wanapuuza, hawaheshimiwi (alama 4) |
| **f) Mathari**<br>**- Elimu isiyo na vitendo ni sawa na mti ambao hauna majani**<br>**- Haumpumzishi yeyote anayekaa chini ya kivuli chake**<br>**- Ni taabu tupu udanganyifu kwa watu** | (alama 3) |
| **g) i) Maulama- Wasomi**<br>**ii) Wameongelewa- Wametukuzwa, wamesifiwa (Alama 2)** | i) Wagatao- wagongao<br>ii) Huwahini- Nyima Kataza (alama 2) |

13. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo: -***

**CHEMA HAKIDUMU**

*Chema hakidumu, kingapendekeza,*
*Saa **ikitimu**, kitakuteleza,*
*Ukawa na hamu, kukingojeleza,*
*Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza.*

*Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,*
*Japo mara tumbi, kinshaniliza,*
*Na japo siombi, kipate n'ongeza,*
*Mtu haniambi, pa kujilimbikiza.*

*Chema mara ngapi, kinaniondoka,*
*Mwahanga yu wapi? Hakukaa mwaka,*
*Kwa muda mfupi, aliwatilika,*

*Ningefanya lipi, ela kumzika?*

*Chema wangu babu, kibwana Bashee,*
*Alojipa tabu, kwamba anilee,*
*Na yakwe sababu, ni **nitengenee**,*
*Ilahi wahhabu, mara amtwee.*

*Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,*
*Hadi siku hini, Yu moyoni mwangu,*
*Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,*
***Ningamtamani**, hatarudi kwangu.*

## ***Maswali***

(a) Eleza dhamira ya mwandishi
(b) Fafanua umbo la shairi hili
(c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari
(d) Taja na kutoa mfano mmoja wa tamathali yoyote ya lugha inayojitokeza katika shairi
(e) Taja mbinu nne za uhuru wa mshairi huku ukitolea kila mbinu mfano

(f) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na vile yalivyotumika**: -
(i) Nitengenee
(ii) Ningamtamani
(iii) Ikitimu

## ***Majibu***

a. Dhamira ya mwandishi ni kuwa chema hakidumu.
b. -Shairi lina beti 5
-Kilau beti una mishoro 4 yenye vipande 2.
-kila mshororo una mizani 6, yaani (6 kwa 6) jumla mizani 12 kila mshororo.
-Shairi limetungwa kutumia bahari ya KIKAI na pia bahari ya UKARAGUNI. (*Zozote 4x1 =4)*
c) Kitu chema hakidumu hata kama kinapendeza, saa yake ikifika kwa kuponyoka ukawachwa na hamu ya kukirejea lakini wapi. Ni vigumu

kwani hauwezekani. (*Alama 4*)

d) Mfano mmoja wowote wa tamathali uliojitokeza katika shairi ni ule wa Balagha/ Istiari/Uhaishaji

*(alama 2)*

e)-Vina vina badilika badilika.

-Idadi ya mizani katika kila mishororo ya ubeti wa shairi hili imepunguzwa kutoka 8 hadi 6.

-Mshororo wa kwanza katika kila ubeti wa shairi hili ni kama kibwagizo au mkarara.

-Neno chema limetumiwa kubainisha maana tofauti.

-Aina ya tarbia lakini limetengeka kikai.

*(zozote 4x1 = 4)*

f) (i) Nitengenee, Niweadilifu / niwe mwema / niwe sawa.

(ii)Ningamtamani – Ningemthamini

(iii)Ikitimu – ikifika (*1x3 = 3)*

14.. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo: -***

*1. Ni sumu, sumu hatari*
*Unahatarisha watoto*
*Kwa ndoto zako zako leweshi*
*Za kupanda ngazi*
*Ndoto motomoto ambazo*
*Zimejenga ukuta*
*Baina ya watoto*
*Na maneno laini*
*Ya ulimi wa wazazi*

*2. Ni sumu, sumu hasiri*
*Unahasiri watoto*
*Kwa pupa yako hangaishi*
*Ya kuwa tajiri mtajika*
*Pupa pumbazi ambayo*
*Imezaa jangwa bahili*
*Badala ya chemichemi*
*Ya mazungumzo na maadili*
*Baina ya watoto na mzazi*

*3. Ni sumu, sumu legezi*
*Unalegeza watoto*
*Kwa mazoea yako tenganishi*
*Ya daima kunywa 'moja baridi'*
*Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu*
*Hadi saa nane usiku*
*Huku yakijenga kutofahamiana*
*Baina ya watoto na mzazi*

*4. Ni sumu, sumu jeruhi*
*Unajeruhi watoto kwa pesa,*
*Kwa mapenzi yako hatari*
*Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa*
*Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi*
*Na kisha kwenye madawa ya giza baridi*
*Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi*

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili
(b) Fafanua maudhui ya shairi hili
(c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta?

(d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mfano
(e) Eleza umbo la shairi hili
(f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari
(g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi;

(i) Giza baridi
(ii) Yanakufunga katika klabu

***Majibu***

a) Kichwa
- Kielelezo kibaya
- Tabia mbovu kwa watoto
- Wazazi wabaya/ walegevu

b) Maudhui ya shairi

- Mshairi anasema kuwa wazazi wanahasiri watoto kwa pupa yao ya kulewa kila wakati na kuwa kielelzo kibaya
- Wazazi kukaa vilabuni mpaka usiku wa manane bila kufahamiana na watoto wao ni vibaya
- Wazazi kuwapa watoto pesa nyingi ni tabia potovu kwani wanazitumia dawa za kulevya
- Wazazi wanatafuta utajiri na kukosa wakati wa kuwashauri/ kuwafunza maadili mema

c) Kinachojenga ukuta

- Hapana mazungumzo ya kishauri baina ya watoto na wazazi nah ii hujenga ukuta baina ya watoto na wazazi
- Kulewa kila wakati na kukaa kilabuni kwa mpaka usiku wa manane hujenga ukuta kwa kuwa mzazi huwa hapati wakati wa kuzungumza na mtoto 2x1=2

d) Tamatahli za usemi

1. Takriri – ni sumu, sumu
2. Tashihisi – ndoto zinajenga ukuta/ yanakufunga katika klabu
3. Istiara – ni sumu
   Kutaja – 1, Mfano – 1

e) Umbo la shairi

- Lina beti nne
- Kila mshororo una mishororo tisa isipokuwa ubeti wa mwisho
- Ni shairi huru kwa kuwa halizingatii arudhi

f) Lugha nathari- ubeti wa nne

- Mshairi anasema kuwa wazazi wanaumiza watoto kwa kuwapa pesa
- Ni vibaya kuliwaza watoto kwa kuwapa pesa
- Kwani huwaingiza katika maovu ya kuvuta sigara na ulevi na mihadarati
- Hali hii inaishia upotofu wa watoto/ huwaingiza katika hali mbaya/ kifo

g) Maana ya vifungu

- Giza baridi – hali mbaya/ kifo

- Yanakufunga katika klabu – kuwa na mazoea mabaya ya kukaa kilabuni kulewa mpaka usiku wa manane

## SAUTI MBALIMBALI ZA WASHAIRI

***WEUSI HUU.***

*Weusi huu weusi, umeniponza si haba*
*Weusi huu weusi, umeninyima kibaba*
*Weusi huu weusi, u nami kwa siku saba*

*Weusi huu weusi, napokonywa tonge langu*
*Weusi huu weusi, kutwa wanipa machungu*
*Weusi huu weusi, ingawa kanipa Mungu*

*Weusi huu weusi, hutamani kuuvua*
*Weusi huu weusi, wanikosesha satua*
*Weusi huu weusi, huchoma kushinda jua*

*Weusi huu weusi, sisemi nikasikika*
*Weusi huu weusi, weusi wa Mwafrika*
*Weusi huu weusi, lini utathaminika?*

*Weusi huu weusi, ni dhiki kwa wanasoka*
*Weusi huu weusi, salata ilopotoka*
*Weusi huu weusi, Majaliwa ya Rabuka*

***Jibril Adam (Abuu Sanaya)***

***MAHASIMU WACHUNGU***

*Nafungua ruhu yangu,ilofungwa kama fungu*
*Nieleze kunga zangu,kwawo penda yangu wengu*
*Waso uso wa maningu,walo nazo hila chungu*
*Sitishwi nyungunyungu,wajapojazia chungu*

*Na wanotumia rungu,kunitisha kwa machungu*
*Wakamila kilo changu,ela kunipa mizungu*
*Ntainuka kwa mawingu,na kushinda zao pingu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu*

*Wanofundika makungu,kwa ufundi nende zangu*
*Wakafunda ndia zangu,maguu angu yanungu*
*Yatawarudi ya nungu,hawatafikila mbingu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu*

*Pingu chungu kwake Mungu,tawa tamu chungu pingu*
*Damu tamu kwawo yangu,tamu damu tamu chungu.*
*Dawa fungwa ya makungu,tawa iso fungwa kungu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu.*

*Wangadaku manzi wangu,asije kuwa mwezi wangu*
*Wangeleta manza kwangu,kuharibu mwezi wangu*
*Wangaruka ni vipungu,hawatofika kwa mbingu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu*

*Nyungunyungu waso nyungu,wanajaza changu chungu*
*Wanafosi jasho langu,na kukila chungu changu*
*Sitowacha ulimwengu,roho yangu i kwa Mungu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu*

*Fungula malango Mungu,wasihule moyo wangu*
*Uyishiye kwa mawingu ,unguzila zao rungu*
*Nipawe mbawa za pingu,wasipate gulu langu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu*

*Namaliza kunga zangu,pa nyasaye pawe pangu*
*Imetika yao myungu,sitishiwi na miungu*
*Wajakwenda kwa mangugu,nitafunga tatu nyungu*
*Sitishiwi nyungunyungu,wajapojazia chungu.*

***WADI SANDICHI***
***( Fakiri wa maweni)***

***<u>KISWAHILI</u>***

## ***<u>NAKUITA</u>***

*Kiswahili nakuita, itika usinyamae, mtu hakatai wito*
*Njoo bila kusita, wala usiniambae, kwangu wewe ni kito*
*Kila upigwapo vita, na kila akuonae, moyo unapata joto*

*Najua umedhiliwa, umekuwa madhulumu, ghalibu umehiniwa*
*Wenziyo wathaminiwa, na wewe wanakusumu, kama mtoto mkiwa*
*Ulivyo mbarikiwa, hili hawalifahamu, laiti wangelijuwa*

*Kwako hakuna badili, kwa hisani ufanyayo, kwa wageni na wazawa*
*Wala hakuna mithali, mwenye hadhi na kufuyo, hakika hajazaliwa*
*Wengi umewafadhili, pasi na kuleta choyo, ama kuzua adawa*

*Hata wangalikutisha, wakubeze kwa dharau, viwavyo wakuumbue*
*Kwangu nakukaribisha, siwezi kukusahau, hili daima ujue*
*Hadhiyo nitapaisha, kwa methali na nahau, dunia ikutambue*
***Jibril Adam (Abuu Sanaya)***

## ***NARUDI NYUMBANI.***

*Nimeshakata kauli, na kuiweka nadhiri*
*Nisharatibu shughuli, nisoweza kuighuri*
*Ingawa yenyewe ghali, yanilazimu safari*
*Nanuia kusafiri*

*Kusafiri ni faradhi, kitalifa na maili*
*Hata yakaja maradhi, nia yangu sibadili*
*Lije lenye kubughudhi, hima nitalikabili*
*Nazidisha tashtiti*

*Narudi kwetu nyumbani, kule nilikozaliwa*
*Ingawa kwetu gizani, ndiko nilikojaliwa*
*Tapita vishorobani, nyayo nikiziambuwa*
*Huko nitapokelewa*

*Miroromo ya bakari, nyuni wakiamkia*
*Ndiyo hunipa fahari, kila nikikuwazia*
*Huniamshia ari, nirudi 'lipotokea*
*Siwezi kumilatia*

*Sakafu zenye samadi, ndivyo zilosakifiwa*
*Vijumba vilosujudi, vya kuvuja vikalowa*
*Ila sioni kusudi, hajivanielemewa*
*Nyumbani kwetu nyumbani*

*Mlenda kwenye sahani, na kiporo cha ugali*
*Kutwa tupo machungani, na mitamba kwa fahali*
*Kisha tukoge mtoni, wala hatukujidhili*
*Ndiko kulikonikuza*

*Basi nawacha magari, na mwanga wa ugenini*
*Sitaki tena kikiri, zinivuazo thamani*
*Nyumbani nishataswiri, na sasa niko mbioni*
*Kuhujuru ugenini*

*Narudi kwetu nyumbani, kilipo kitovu changu*
*Nimeshatia imani, na kumsabihi Mungu*
*Naweka begi begani, macho yatazama mbingu*
*Narudi kwetu nyumbani.*
***Jibril Adam (Abuu Sanaya)***

***MOYO.***
*Mtima wangu tulia,kwa hiki changu kifua*
*Acha kutamania,kila kitu kwa sinia*
*Usione vyaelea,ukataka kuchukua*
*Ninakuomba tulia,tulia moyo tulia.*

*Masketi yakipita,usije niangaisha*
*Usiniletee vita,lau ukaniangusha*
*Uwache kuchotachota,uwache kuniabisha*
*Ninakuomba tulia,tulia moyo tulia.*

*Miguu inayong'ara,wataka kuangalia*
*Unanipa mafikira,wanifanya naumia*
*Hata nikiona sura,hautaki kutulia*
*Nakuomba moyo wangu,tulia moyo tulia*

*Niko shuleni tulia ,wacha nisome tulia*
*Wakati ukifikia,ndo uanze kusumbua*
*Sasa wacha kupepea,ungali bado tulia*
*Nakuomba moyo wangu,tulia moyo tulia*

*Wacha kudundadunda,kwa kukiola kifua*
*Acha ipite marinda,uwache kunishitua*
*Kwa nini unajipinda ,na kuniletea nia*
*Nakuomba moyo wangu,tulia moyo tulia*

*Nikitazama kiuno,unanijaza fikira*
*Waniletea maono,ya kutaka kuchakura*
*Wataka niwe sindano,unipatie hasara*
*Nakuomba moyo wangu tulia moyo tulia*

*Wanituma kwa sukari,hata ikiwa ni chungu*
*Unanipa nyingi hari,wanichemsha maungu*
*Sukari huwa shubiri,nisikize moyo wangu*
*Nakuomba moyo wangu,tulia moyo tulia*

*Ewe mola ulo mbingu,shika uno moyo wangu*
*Utulize moyo wangu,usikie ombi langu*
*Nisiyapate machungu,shida zote zije kwangu*
*Ninakuomba tulia,tulia moyo tulia.*
***WADI SANDICHI (****FAKIRI WA MAWENI)*

## ***MWANA MTUKANA NINA.***

*Mwana mtukana nina, ni mwana mlaaniwa*
*Atende kila aina, hawezi kufanikiwa*
*Hapati yalo mwanana, mazuri hupungukiwa*
*Uchao husumbukana, katu si mbarikiwa*

*Heri kumfuga mbuzi, mnyama mwenye mafao*
*Kuliko mwana jambazi, akawa ndiye mwanao*
*Akaungana na wezi, awe kwenye wauao*
*Huyo si mwana azizi, hadhi yake ni masuo*

*Husemwa mwana mgomvi, heshi kukipatapata*
*Asotii wenye mvi, huwa mwingi wa kujuta*
*Mwana mpenda uchinvi, waadhi asokamata*
*Mdharau wala chumvi, msibani hujikuta*

*Mwana aso msikivu, mtundu bila mithali*

*Mwana mpenda uvivu, idili asiyejali*
*Mwana alo mlegevu, katika kila amali*
*Huwa mwana mpumbavu, zuzu aso na akili*

*Mwana aso masikizi, ni mwana mbadhirifu*
*Ni mwingi wa mapuuzi, si mwana muangalifu*
*Humbughudhi mzazi, kwa kukosa ukunjufu*
*Mwisho hulowa machozi, kwa mawi yalo lufufu*

*Mwana asiye idili, si mwana mwenye baraka*
*Hujipa yenye muhali, hapati anachotaka*
*Kipato chake kalili, asopenda kuchanika*
*Ni mchache wa shughuli, na mwepesi wa kutaka*

*Mwana mpenda anasa, tangu hana mwisho mwema*
*Anasani hujitosa, mwisho akose salama*
*Mumo munayo mikasa, hima ikamsakama*
*Adhama akiigusa, mara huzuka lawama*

*Mwana aso mcha Mungu, ni mwana mwenye hasara*
*Asozitazama mbingu, na mwezi unapong'ara*
*Adhabu yake ni chungu, tena haina kafara*
*Keshajibana kwa pingu, mbele yake Al- Ghaffara.*
***Jibril Adam (Abuu Sanaya)***

## ***MIHADARATI NI SUMU***
*Maozi yamelegea, kwenye darasa haoni,*
*Mwalimu ang'ang'ania, kufundisha ubaoni,*
*Somo halitatimia, kuna moshi akilini,*
*Mihadarati ni sumu, kijana kuwa makini.*

*Shuleni hajatulia, muda wote yu mbioni,*
*Ataka kujipatia, ana kiu mdomoni,*
*Apate kujisikia, ametulia kitwani,*
*Mihadarati ni sumu, kijana kuwa makini.*

*Akisha kuzitumia, ni silaha mkononi,*
*Kazi kujitutumua, ana nguvu kifuani,*

*Kumbe hafikii mia, wala hata hamsini,*
*Mihadarati ni sumu, kijana kuwa makini.*

*Hana cha kujivunia, anabaki laitini,*
*Mitihani ikijia, hafikii ishirini,*
*Alama anazozoa, ni matope mtaroni,*
*Mihadarati ni sumu, kijana kuwa makini.*

*Pesa akizipokea, hazikai mfukoni,*
*Mzazi amtumia, kumtilia imani,*
*Kumbe zinapotelea, kwa walevi mangweni,*
*Mihadarati ni sumu, kijana kuwa makini.*

*Mtumiaji sikia, urejee kwenye dini,*
*Mungu akuangalia, umetiwa hisabuni,*
*Badili yako tabia, utaingia peponi,*
*Mihadarati ni sumu, kijana kuwa makini.*

***Uledi Brian Rop***

## ***NYOKA WA NDUMAKUWILI***

*Binadamu vimelea, watu hawatabiriki,*
*Leo anakuchekea, mkate mkishiriki,*
*Kesho atakukemea, ja mke akutaliki,*
*Nyoka wa ndumakuwili.*

*Huuma akivuvia, nyoka wa ndumakuwili,*
*Huku anakusifia, muwazi kama kandili,*
*Sifa anazomwagia, nyingi isiyo kalili,*
*Nyoka wa ndumakuwili.*

*Ina mema na maovu, huu ndio ulimwengu,*
*Ina maji na pakavu, penye amani na bangu,*
*Wapo walio chakavu, gambani miba za nungu,*
*Nyoka wa ndumakuwili.*

*Tahadhari mahuluku, kaa nao kimtindo,*
*Husiana kisukuku, mtu pweke ni uvundo,*
*Hawapendi uwapiku, cheo ukiweke kando,*
*Nyoka wa ndumakuwili.*

***YUWAPI***

*Yu wapi mwenye kasumba, ajuaye itikadi,*
*Asiyekuwa mwembamba, mnene anifaidi,*
*Ambaye mungu kaumba, kitwa hadi kisugudi,*

*Yuwapi mruka kamba, asokuwa mkaidi,*
*Kilaza hawi mchumba, kulala kifudi fudi,*
*Huku akisema kwamba, mume atalipa kodi.*

*Yuko wapi jike simba, yule mwenye kushitadi,*
*Asusaye pumba pumba, au zawadi zawadi,*
*Mavaziye ni mtumba, na kaniki ikibidi.*

*Yuwapi asiyeomba, bebi n'tumie kadi,*
*Ajuaye pamba nyumba, ubani pamwe na udi,*
*Kimpata ni mpemba, nayo itakuwa sudi.*

*Yu wapi mkaa shamba, kwa mama apige hodi,*
*Kwa udi pia uvumba, naye afanye akidi.*
*Alo na ngozi ya mamba, akae hadi nirudi.*

***Uledi Brian Rop***

***TESA UKIWA KIJANA***

*Nazuka na mada pana, kuwapa usia nyiye,*
*Pulikani nayonena, maasa yana memaye,*
*Nakwamba uli kijana, nawewe siti bibiye,*
*Tesa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

*Utungu wa kila mwana, ajuaye mzaziye,*
*Haswa haswa niye nina, huumwa sana ninaye,*
*Kwanda kadiriya kina, cha maji ili ungiye,*
*Tesa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

*Tesa ukiwa kijana, utaliya baadaye,*
*Mnwa tembo mvulana, huharibu maishaye,*
*Sigara bangi haina, starahe kwa avutaye,*

*Tesa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

*Kuzurura kila kona, hapa kule upo weye,*
*Yeyote mkikutana, kwamba unazuka naye,*
*Vya haramu mkipana, ukidhani kuwa ndiye,*
*Tesa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

*Tuko lako msichana, kupa yeyote ajaye,*
*Wa leo siye wa jana, na wa jana leo siye,*
*Yeyote mkikutana, kwamba unazuka naye,*
*Tesa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

*Ngoma ikipigwa sana, hupasuka hatimaye,*
*Juwa ni moshi ujana, vizuri ujiandaye,*
*Kesho yake utafana, maishayo ya keshoye,*
*Tesa ukiwa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

*Cha ziada miye sina, sina cha ziada miye,*
*Majuto kama laana, hukupiga kinyumaye,*
*Maradhi yakikazana, ni wewe uuguaye,*
*Tesa ukiwa kijana, uzee utakutesa.*

***Uledi Brian Rop***

## ***NAKUPA***

*Nakupa roho na mwili, wende nazo uendako,*
*Penzi limenikabili, nikiwa kandoni pako,*
*Menifunga silisili, sikomi vionjo vyako.*

*Wapendeza ja mdoli, napapasa juu yako,*
*Waama una kibali, kutoka kwa mola wako,*
*Wala hikuwa ajali, kulipata pendo lako.*

*Nakomolea kufuli, kurejea nyuma mwiko,*
*Walodhani si muhali, nimeondokea soko,*
*Sasa natulia tuli, pasina msukosuko.*

*Wapiganapo fahali, nyasi hwona fadhaiko,*
*Nasi tutie akili, tusije zivunja miko,*

*Tupendane kulihali, wale tusiwape cheko.*

*Sifanyi kama dalali, minawe sako kwa bako,*
*Hatima nimehafili, kumaliza mzunguko,*
*Hongera kwayo tunguli, na huyo mganga wako.*

***Uledi Brian Rop***

***SOMA MWANA.***

*Kusoma mwana si adha, kesho usije jikwae*
*Maisha yana bughudha, soma ujuzi utwae*
*Takurithi hata fedha, ila soma ujifae*
*Soma nakusihi soma, elimu uipakatete.*

*Kila siku tafakari, changamoto za maisha*
*Rauka alfajiri, taa mwana kuziwasha*
*Ingawa ni kibatari, kesho kitanufaisha*
*Soma nakusihi soma, ujana huu ni moshi*

*Soma usiwe mlofa, ukapate yako mali*
*Utapata na maarifa, kujijenga kiakili*
*Ujenge lako taifa, uikweze yake hali,*
*Tafadhali mwana soma, maishani sisumbuke.*

*Utafunzwa maadili, kuishi vyema na watu*
*Jifunze uwe wakili, uwafae wengi watu*
*Tena ukawabadili, wa tabia zenye kutu*
*Masomo muhimu kweli, yatazidi kukuumba*

*Soma siku za usoni, elimu ikawe ngao*
*Soma uwe wa thamani, kesho uwe tegemeo*
*Wenza uwatoe chini, wakuone pembejeo*
*Yashike ninayonena, kwa bidii soma mwana.*

*Yatakupa ujasiri, uweze kujiamini*
*Masaibu yakijiri, ujitoe mtegoni*
*Upesi utafakari, utatue kwa makini*

*Nenda shule ukasome, usijitie ajizi*

*Beti saba zatimia, elimu ina amana*
*Yote nilokuusia, ni mambo yenye kufana*
*Na dua nakuombea, akukimu Maulana*
*Soma nakusihi soma, maishani hutojuta.*

***Francisca Wambua (Kalamu isiyochoka)***

***NDOA ZA KISASA.***

*Ninakutuma barua, someka na wengi watu*
*Nenda pasi kuhofia, waulize wanakwetu*
*Jibu nalisubiria, umeshawatoka utu*
*Mbona ndoa za kisasa, si kama zile za zama?*

*Sio kama za zamani, ndoa zilizotukuka*
*Zilizopewa thamani, zikawa zaheshimika*
*Hazikuwa za gizani, zilizojawa dhihaka*
*Hizi ndoa za kisasa, hazidumu huvunjika.*

*Zajiri na kutoweka, kama ilivyo misimu,*
*Zimejaa hekaheka, ndoa zisizo utamu,*
*Ndoa zisizoongoka, zimeshitadi haramu,*
*Hizi ndoa za kisasa, Hubarikiwa na nani?*

*Japo kaziumba Mola, ndoa sasa zina doa*
*Ndoa zimepata ila, wanandoa waugua*
*Ziwapi za zama mila, nani atazingatia*
*Yakini ndoa za leo, zimekosa muamana*

*Ni ua la kunyauka, ambalo si maridhia*
*Haibaye huchujuka, likakosa kuvutia*
*Haliwezi tamanika, vijana wanasusia*
*Mbona ndoa za kisasa, zimejawa usaliti?*

*Zimejawa usaliti, wengi wanafarakana*
*Nyingi zina umauti, vifo vinarundikana*

*Ya nini ndoa za vyeti, bila kuaminiana*
*Kweli ndoa za kisasa, zimejawa walakini.*

*Zimejawa walakini, nyingi ni za kipato*
*Iwapo huna mapeni, utapata kung'uto*
*Kwa masuto hadharani, utawachwa kwa majuto*
*Kweli ndoa za kisasa, hazina hata mashiko.*

*Hazina hata mashiko, wala cha kujivunia*
*Wanandoa mbwakoko, ndoa wanajivunjia*
*Nyingi zina sokomoko, kila siku wanalia*
*Hizi ndoa za kisasa, Mola zitatumaliza?*

*Tuundieni kamati, ili tupate majibu*
*tuondowe vizingiti, ziwe kama za mababu*
*Ziwe ndoa zenye dhati, zisiwe za kusulubu*
*Ndoa za sasa adhabu, nasi ni waadhibiwa?*

***Francisca Wambua (Kalamu isiyochoka)***

***KIJANA.***

*KIJANA*
*Furaha unaninyima, hadi lini nisubiri?*
*Daima waniandama, na kuninywesha shubiri*
*Moyoni unanichoma, nasema isiwe siri*
*Kwa nini wanipa tabu, naomba nipe likizo!*

*NJAA.*
*Hodi kwako sikubisha, mwenyewe kanialika*
*Sikuja kujishengesha, mbona unalalamika*
*Leo hili nakupasha, lishike nalotamka*
*Uvivu ungeukoma, kwako mie ningetoka.*

*KIJANA.*
*Maskini kazi sina, sina pa kujiokoa?*
*Chuoni nilikazana, ingawa sikutoboa*
*Nilopanda sikuvuna, yalosalia mabua*
*Mbona zinifike tabu, naomba nipe likizo!*

*NJAA.*
*Mwenyewe wajichongeya, limaizi kwanza hili*
*Huwachi kuwayawaya, waranda kila mahali*
*Maisha wayapapiya, hushiki moja shughuli*
*Uvivu ungeukoma, kwako mie ningetoka.*

*KIJANA.*
*Ofisini ngojangoja, kila mara wanijibu*
*Jiji lenyewe ujanja, daima laniandhibu*
*Vipi nizikidhi haja, yanifwata majukumu*
*Mbona zinifike tabu, naomba nipe likizo!*
*NJAA.*
*Chuoni mwana kaenda, ujinga kuuondowa*
*Ila bado kakuganda, akilini umejawa*
*Lolote waweza tenda, kwa ujuzi ulopewa*
*Uvivu ungeukoma, kwako mie ningetoka!*

*KIJANA.*
*Nielewe tafadhali, kazi zimeadimika*
*Pengine niende mbali, mbali huko Amerika*
*Kuna kazi afadhali, hadhi yangu hitoshuka*
*Mbona zinifike tabu, naomba nipe likizo!*

*NJAA.*
*Viwandani mna kazi, si lazima ofisini*
*Nipe yako masikizi, nikutoe ujingani*
*Kikosa kuyamaizi, utafia ukatani*
*Uvivu ungeukoma, kwako mie ningetoka!*

*KIJANA.*
*chochote nifanye eti, nilichosoma chuoni!*
*Uzamifu n'acho cheti, nende vipi viwandani?*
*Kachafue zangu suti, kwa kazi ziso thamani*
*Mbona wanipa taabu, naomba nipe likizo.*

*NJAA.*
*Bandani mwako sihami, daima nitakuponda*
*Kwa makeke naja mimi, kutwa takudundadunda*

*Nikufunze kujihami, kazi zote kuzitenda*
*Uvivu ungeukoma, kwako mie ningetoka.*

*KIJANA.*
*Kijana niko tayari, kuyakoma ya kipuzi*
*Ya kwako natafakari, hakika kazi ni kazi*
*Kujikaza ndiyo siri, ya njaa nyumba ajizi*
*Mbona wanipa taabu, naomba nipe likizo.*

*NJAA.*
*Nami njaa takwondoka, kitenda ulitoapa*
*Huwezi tena kuniweka, haki yangu ukinipa*
*Tayari shapapatuka, kwako mie nimehepa*
*Uvivu ungeukoma, kwako mie ningetoka.*

***Francisca Wambua (Kalamu isiyochoka)***

***SIASA ZITAPITA TU!***

*Kalamu ninachukua, kuamba yalo moyoni*
*Zani tusije zizua, zikatutia motoni*
*Amani twajivunia, vijijini na mijini*
*Siasa ni kama wingu, hutanda na kutanduka*

*Tangu zama za zamani, tumeishi kwa amani*
*Ila leo ukubwani, twazozana hadharani*
*Si vizuri asilani, sisi sote majirani*
*Siasa ni kama wingu, hutanda na kutanduka*

*Lipi tunajivunia, kwa vurugu mitaani*
*Visasi twajiwekea, nayo makovu moyoni*
*Ya nini basi ghasia, huku kwetu mashinani?*
*Siasa ni kama wingu, hutanda na kutanduka*

*Tangu jadi tumekua, tukiishi kwa amani*
*Undugu wa kuvutia, leo mbona usononi*
*Husuda zatukolea, na kutunyima amani*
*Siasa ni kama wingu, hutanda na kutanduka*

*Wana wetu wanakua, wajionea machoni*

*Kutwa tunavyowania, kwa vurugu mitaani*
*Nakuombeni sikia, mwajidhili hadharani*
*Siasa ni kama wingu, hutanda na kutanduka*

*Twataka kufurahia, tuwapo uchaguzini*
*Umpendae chagua, wala usizue zani*
*Toka moyoni amua, pesa zisikurubuni*
*Siasa zni kama wingu, hutanda na kutanduka*

*Leo ninawausia, naitangaza amani*
*Vigogo waje sikia, wito wetu hadharani*
*Waishi wakiyajua, nia yetu aushini*
*Siasa nikama wingu, hutanda na kutanduka*

*Kadi tama ninatua, kalamu naweka chini*
*Kura zinakaribia, hima tufanye makini*
*Ujirani ni mafua, yasokoma aushini*
*Siasa ni kama wingu, hutanda na kutanduka*

***Francisca Wambua (Kalamu isiyochoka)***

## ***CHAGUA MAENDELEO***

*Ya mgambo imelia, hodihodi naingia*
*Ule muda 'mewadia, ya kura kuwapigia*
*Wa kukufaa chagua, siku hiyo 'kiwadia*
*Uongozi sio chama, chagua maendeleo*

*Waziwazi nawambia, hili sitanyamazia*
*Siku hiyo raukia, wa manufaa chagua*
*Kwenye foleni salia, zamu yako 'tatimia*
*Uongozi sio chama, chagua maendeleo*

*Kweli tumeambulia, kwa wale wasio nia*
*Kwa muda tumeumia, siwezi kusimulia*
*Kosa ni kulirudia, kuchangua haramia*
*Uongozi sio chama, chagua maendeleo*

*Mijini hupotelea, raha wakijipatia*
*Magari watembelea, nasi tukijililia*

*halafu watatujia, na hela kutuvutia*
*Uongozi sio chama, chagua maendeleo*

*Mitini wameingia, yetu wamepuuzia*
*Mitano ikitimia, wakumbuka kutujia*
*Hatua tutachukua, afisini kuwatoa*
*Uongozi sio chama, chagua maendeleo*

*Beti sita nadondoa, wosia kuwapatia*
*Busara nawagawia, ili msije jutia*
*Yapasa kuzingatia, tusambe hatukujua*
*Uongozi sio chama, chagua maendeleo*

***Francisca Wambua (Kalamu isiyochoka)***

## JOHARI

*Natunga hini nudhumu, niambe yalo dhahiri*
*Tena yenye umuhimu, muyaonee fahari*
*Utungo wenye kudumu, Sasa na hata dahari*
*Hili kwenu ni johari, kwa wapenzi wa utunzi*

*Hili kwenu ni johari, kwa wapenzi wa utunzi*
*Nitatunga kwenye Shari, hata mtie mizizi*
*Dawamu ninayo ari, wala sina ajaizi*
*Tunu hii ninawapa, mhifadhi kwa makini*

*Tunu hii ninawapa, mhifadhi kwa makini*
*Wosia wangu nawapa, walozama utungoni*
*Tuzamie kama papa, hadi pale ufukweni*
*Pale tutavikwa taji, ya sanaa ya utunzi*

*Hakuna alobobea, kichango twachangizana*
*Leo wanaosifika, mwanzoni waling'ang'ana*
*Ndio wanaotajika, kwa kazi zilizofana*
*Usione gere kaka, nyota yako i njiani*

*Zawadi huzawadiwa, anayeibuka bora*
*Kwenu mliojaliwa, shikeni tahadhara*

*Mjivunie vipawa, msitunge za uchwara*
*Zawadi hino nawapa, enyi mashabiki wangu*

*Sita ninatamatisha, nalikunja langu jamvi*
*Iwe tunu ya maisha, hata muwe nazo mvi*
*Koja hii nawavisha, mzidipo kula chumvi*
*Tuzo nawatunukia, Malenga Mtanashati*

***Momanyi Henry Rioba (Malenga Mtanashati)***

**NIWEPO**

*Naiona siku moja, furaha iso kifani,*
*Kwa hamumu naingoja, ilojaa tumaini,*
*Nataka mimi niwepo.*

*Niwepo kushuhudia, mafisadi wakinyongwa,*
*Mbele ya wote insia, majeneza yakifungwa,*
*Nataka mimi niwepo.*

*Niwaone majangili, wanotuulia tembo,*
*Kwa kutaka mengi mali, wakitobolewa tumbo,*
*Nataka mimi niwepo.*

*Wauza mihadarati, siku yao itafika,*
*Nitaona ithibati, motoni wakichomeka,*
*Nataka mimi niwepo.*

*Nitacheka wanyang'anyi, wa kudhulumu fukara,*
*Hata pia wasengenyi, wakitolewa kafara,*
*Nataka mimi niwepo.*

*Wajutie wauwaji, kosa wakiadhibiwa,*
*Nao wote wakosaji, mpopota kigongewa,*
*Nataka mimi niwepo.*

*Nitahongera wazuri, wale wapendao utu,*
*Watavikwa utajiri, na wamete metumetu,*

*Nataka mimi niwepo.*

***Allan Lumanyasi Chevukwavi (Mwoshashombo)***

## ***UFAIDIKEJE?***

*Unisimange mabaya, heshima kunichafua,*
*Hadharani bila haya, kudanganya wendelea,*
*Yangu wapenyea taya, kwa uongo kunenea,*
*Ndipo ufaidikeje?*

*Nikosane na rafiki, kwa huo wako umbea,*
*Anione ni nafiki, kwa fitina kutolea,*
*Mbona huo uzandiki, watu kuchanganishia?*
*Ndipo ufaidikeje?*

*Niwe mja upwekeni, kwa ndoa kunivunjia,*
*Nikose mke nyumbani, ndiwe umemchochea,*
*Nikiwa mfano duni, niikose familia,*
*Ndipo ufaidikeje?*

*Fulusi unilaghai, ukope na kupotea,*
*Simu zangu hupokei, kuzidi wanizimia,*
*Mbona basi huongei, pengine nakuachia?*
*Ndipo ufaidikeje?*

*Uende kilingeni, majini kunitumia,*
*Niwe mtu punguani, na mararu kutembea,*
*Nile vitu vya pipani, niishi nikiumia,*
*Ndipo ufaidikeje?*

*Ya nini kunidanganya, maovu kunitendea,*
*Kizani unanifinya, mchana wanichekea,*
*Mbona ujifanye panya, kuuma kipulizia?*
*Ndipo ufaidikeje?*

***Allan Lumanyasi Chevukwavi (Mwoshashombo)***

## ***NAJIHUKUMU***

*Naanza tunga utenzi,*
*Unaohusu majonzi,*

*Nilivyofanya ushenzi,*
*Maisha yakapotea.*

*Nilikuwa nimepanga,*
*Naende tafuta unga,*
*Matatizo kunisonga,*
*Iwapo yangepungua.*

*Nilikuwa na sabini,*
*Nauli ya safarini,*
*Ningelipia garini,*
*Ja wengine abiria.*

*Kabula kutoka kwangu,*
*Nikamwomba wangu Mungu,*
*Anipe la kwangu fungu,*
*Niingie kibarua.*

*Nikatoka na imani,*
*Kwelekea stanini,*
*Nipande kwenda mjini,*
*Bahati kujaribia.*

*Kupita Mombasa rodi,*
*Barabara maridadi,*
*Basi kiwa kwa spidi*
*Maloli nimefungua.*

*Nikamwona chokoraa,*
*Mmoja alolemaa,*
*Msaada kiombea,*
*Kwa wale wapati njia.*

*Matope akarushiwa,*
*Nguo akachafuliwa,*

*Bila pole kuambiwa,*
*Machozi kajililia.*

*Nikaingiwa huruma,*
*Kwona akijisukuma,*
*Sikuipenda hujuma,*
*Nikataka mchangia.*

*Kono langu kwa kibeti,*
*Nikaliingiza kati,*
*Nimpe japo katiti,*
*Pili kujinunulia.*

*Kwa kuwa nisingeshuka,*
*Kwa sababu ya haraka,*
*Nilimwita kaitika,*
*Pesa nikamwangushia.*

*Nikiwa hapo nilipo,*
*Na basi lingali papo,*
*Akaja mbaya pepo,*
*Mkasa ukatokea.*

*Ndugu yule akisota,*
*Vipeni kuviokota,*
*Matatu ilimkuta,*
*Uhaiwe kuutwaa.*

*Hakika najilaumu,*
*Kumwagisha hiyo damu,*
*Singatoa darahimu,*
*Mauti asingepokea.*

*Litaka kusaidia,*
*Kumbe kifo nachangia,*
*Mimi najilaumia,*
*Anisamehe Rabia.*

***Allan Lumanyasi Chevukwavi (Mwoshashombo)***

## 6. ***SAUTI YA CHANGUDOA.***

*Mwenzenu nafikiria, nashindwa kuvumilia,*
*Kila siku ninalia, chumbani hujifungia,*
*Ila leo nawambia, kila mja kusikia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni mambo haya.*

*Jamani najililia, machozi kujifutia,*
*Moyo nawafunulia, ya nyuma niloishia,*
*Mja niliteketea, mikononi mwa mamia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni mambo haya.*

*Mamangu kajizalia, hala hala nikakua,*
*Siku hiyo kajifia, huyu wangu maridhia,*
*Majonzi yakanijia, kutwa najihurumia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni mambo haya.*

*Babangu akanilea, hadi muda kuwadia,*
*Shuleni kajiendea, paka darasa sitia,*
*Tandatu lipofikia, baba pia kajifia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Kawa mwisho kanyagia, ile ya sikuli ndhia,*
*Kwa nyanya kajiendea, kuishi kwake sikia,*
*Nyanyangu kaniridhia, na chumba kanitengea*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Wajomba kanichukia, fitina kanitilia,*
*Wivi kanisingizia, wa shilingi moja mia,*
*Nyanya kanidhihakia, hasira kanivalia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Giza lipokaribia, wajomba kanitishia,*
*Nitoe shilingi mia, la sivyo 'tajiharia*
*Zana kanikusanyia, kanipiga nakwambia*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Mjini nikaingia, kwa mja msamaria,*
*Nauli kanilipia, ya shilingi tatu mia,*
*Mjini nikatembea, na moyo wajililia*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Giza lilipoingia, usingizi linijia,*
*Kibandani kaingia, kujihifadhi sikia,*
*Wezi kanifumania, kapa kunisaidia*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Tena nilijistabia, tendo walonifanyia,*
*Linilaza kwa zulia, wakanipasua njia,*
*Ubikira kanishia, nikabaki mi nalia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa Chaya.*

*Subuhi lipowadia, njiani nilitembea,*
*Na damu mejigandia, mapajani nakwambia,*
*Kazi nikiulizia, kushotoni na kulia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa Chaya*

*Karibu nikasikia, nyumba ya kumi tisia,*
*Kwa bashasha kaingia, nikimuomba Jalia,*
*Bi kanichangamkia, pale nilipojongea,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa Chaya*

*Kazi akanipatia, ya bia kumuuzia,*
*Jioni ikiwadia, anipe shilingi mia,*
*Watu kawahudumia, na yaangu safi nia*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Siku moja nanywa bia, msichana kanijia,*
*Kwa meza kakaribia, kanishawishi sikia,*
*Kazi atanipatia, niache ile ya bia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Eti akaniambia, malazi 'tanipatia*

*Tena bure bilashia, bila yangu sumunia,*
*Kumbe danguro ningia, utu wangu kupotea,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Maisha kanitishia, lipotaka kukimbia,*
*Mwisho kajiamulia, na nguo kuyavulia,*
*Nikaacha na kulia, wanaume kuchukia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Asali kajirambia, hiari yangu sikia,*
*Na pesa kajipatia, 'ta zile za Tanzania,*
*Hata utu kupotea, sikujali nakwambia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

*Siwezi kuendelea, na hii historia,*
*Mwenzenu ninaumia, moyo wangu unalia,*
*Namini tanijalia, Mola kwa hii dunia,*
*Mwaniita changundoa, tambueni kisa chaya.*

## ***MAPENZI YA UJANANI.***

*Mimi hodi ninabisha, na mlango mfungue,*
*Niulize mino kisha, mnipe jibu nijue,*
*Yamekuwa yanatisha, ya mapenzi mtambue*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Juzi jana mahabubu, leo kesho hayawani,*
*Wanileteа aibu, tena wewe kisirani,*
*Wanitia masaibu, wewe kweli ni haini*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Nakupenda mdomoni, bali moyoni haupo,*
*Sikuachi asilani, labda atage popo,*
*Ni uongo ukazini, bali hisia hazipo,*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Watahamia kwa babu, ikikonda pochi yako,*
*Mbele yao tawa bubu, tena uwe mbwa koko,*
*Moyoni tapata tabu, mana yeye mewa mwiko,*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Namtunza hani wangu, kumbe mkengwa natunza,*
*Fulani atunza wangu, kimtoa hata funza,*
*Watafunga eti pingu, na maisha kuyaanza,*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Kumpata akupendaye, ni ya masika jangwani,*
*Ila akudanganyaye, kumeza maji kooni,*
*Utataka awe ndiye, haiwezi asilani,*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Ataja kurairai, ndani ataka wo uke,*
*Maneno ya kilaghai, mejaa kinywani mwake,*
*Kidanganyika kutii, takupata ende zake,*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Pochini yamehamia, nasikia siku hizi,*
*Masikini waumia, kwa kuikosa hirizi,*
*Kutwa kucha wanalia, kwa dhuluma waziwazi*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Chaniudhi kisa hiki, cha rijali na ajuza,*
*Kajitia hafunguki, hapo mwanzo wa baraza,*
*Kwa ajili ya riziki, ujanawe kauuza,*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

*Kuwaaga sina budi, aheri ya kuonana,*
*Lakini muniahidi, jawabu nitaliona,*
*Kinyamaza nitarudi, niwakumbushe kingwana*
*Mapenzi ya ujanani, yasomewa chuo kipi?*

***PESA.***

*Nawauliza wangwana, hili swali kwa makini,*
*Nimefikiria sana, sa naliweka mezani,*
*Hata usiku wa jana, sikulala asilani,*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani?*

*Kija kijana tajiri, wazee wanasimama,*
*Kija mzee fakiri, wao kwa viti hukwama,*
*Nashangaa sio siri, nani apewe heshima,*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Hino pesa kitu gani, wangwana niambieni,*
*Imewatia dhambini, wanasubiri motoni,*
*Kiambiwa ya peponi, wanayapuza jamani.*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Mandugu wanauwana, kwa tamaa yayo pesa,*
*Walozi wanarogana, na kujiuza vipusa,*
*Wapenzi kunyang'anyana, ndo mtindo wa kisasa,*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Swala la mapenzi jama, si vijana twaonewa,*
*Baba tulia na mama, vijana si tutaowa,*
*Tena sinitie homa, achana na Mwanahawa,*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Vyeti bandia fisini, sio jambo la ajabu,*
*Kila siku ni kazini, wala hawana aibu,*
*Hawamjui Manani, atawatia adabu,*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Kila siku wanasoma, si kuongeza elimu,*
*Pesa yawatia homa, kila siku ni kalamu,*
*Fukara ana lawama, wasomi wamshutumu*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Wana kiu ya daima, hawatosheki kabisa,*
*Wako mbioni nasema, maskini ni mkosa,*

*Hata na wale vilema, wanaisaka kwa sasa*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Unga na bangi nchini, sio pwani wala bara,*
*Vyaingia bandarini, kwa usalama imara,*
*Vinavutwa hadhaarani, si gamu wala sigara,*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

*Hino pesa ni hakimu, inahukumu wangwana,*
*Katiba sio muhimu, yahujumiwa kwa sana,*
*Sitoacha kulaumu, wamenisinya nanena*
*Jamani jama jamani, hino pesa kitu gani.*

## ***NDOTO YAKO***

*Ninasafisha ukumbi, Napenya kwenye Jukwaa*
*Macho yangu siyafumbi, Nisonge bila kukwaa*
*Nakitifua kivumbi, natamba na kutambaa*
*Ndoto yako ni dhahabu, Jamani zidisha moto*

*Jamani zidisha moto, Daima uwe wawaka*
*Wa kuitimiza ndoto, na yote unayotaka*
*Ujipatie kipato, Pa heshima kupafika*
*Ndoto yako ni dhahabu, Masomo ndio migodi.*

*Masomo ndio Migodi, Vitabuni kupachimba*
*Chuoni kabishe hodi, bila kiburi kuvimba*
*Kulipa karo na kodi, Usihofu kama simba*
*Ndoto yako ni dhahabu, kote kote itafute.*

*Kote kote itafute, Shuleni na kwenye kazi*
*Sigara usizivute, mihadarati si ngazi*
*Akilini usifute, Ndoto zako weka wazi*
*Ndoto yako ni dhahabu, tele inayo thamani.*

*Tele inayo thamani, ndoto yako kesho yako*
*Kila unalotamani, tafuta huku na huko*
*Ualimu urubani, utakuletea cheko*

*Ndoto yako ni dhahabu, Soma sana bila shaka.*

*Soma sana bila shaka, upate unachotaka*
*Wala usiwe haraka, kwani haina baraka*
*Pole pole utafika, masomo yana fanaka*
*Ndoto yako ni dhahabu, Vumilia ule mbivu*

*Vumilia ule mbivu, tanga na jua kujua*
*Tulia kwa usikivu, mawaidha kuchukua*
*Usikubali uvivu, Tatizo lako tatua*
*Ndoto yako ni dhahabu, Na akiba haiozi.*

*Na akiba haiozi, usikose kuwekeza*
*Japo kwa shida na chozi, pole pole utaweza*
*Kupata karo ya kozi, biashara kuijaza*
*Ndoto yako ni dhahabu, hata iwe ni kujenga.*

*Hata iwe ni kujenga, jumba nzuri la fahari*
*Sambamba ukijipanga, 'tajenga kwenye bahari*
*Malengo unayolenga, timiza kwa umahiri*
*Ndoto yako ni dhahabu, jithamini jiamini.*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***VIPAJI***

*Shukuru sana Karima, kukupatia kipaji*
*Upande nacho milima, popote upate taji*
*Mezani chaleta sima, kukukimu mahitaji*
*Wa kipaji husimama, Kipaji kina mtaji.*

*Huwezi kukiazima, maalumu kwako gwiji*
*Upande nacho milima, kuibiwa sitaraji*
*Kwa wengine kitazima, Mola pekee mpaji*
*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji.*

*Kitumie kwa hekima, Kwenye miji na vijiji*
*Upande nacho milima, kwa ujenzi ni saruji*
*Kidumishe kwa heshima, kiburi hakifariji*

*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji*

*Kipaji kina hatima, maishani chipuaji*
*Upande nacho milima, 'sijifanye mjuaji*
*Mila zetu za heshima, Zipatie uvaaji*
*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji.*

*Japo kinazo gharama, hasa kwenye utunzaji*
*Upande nacho milima, uitafute siraji*
*Chochea yako karama, Mti nyunyuzia maji*
*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji*

*Usipende kulalama, Jitwike upambanaji*
*Upande nacho milima, Kama chuma mfuaji*
*Juhudizo kutozima, uwe mbele mkuaji*
*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji.*

*Umilisi hima hima, uongeze kwa kipaji*
*Upande nacho milima, ung'are kwa ufaaji*
*Masomoni kugandama, ujuzi umilikaji*
*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji*

*Kipaji kiwe cha kusema, mfano utangazaji*
*Upande nacho mlima, hata kiwe uchoraji*
*Kuigiza kwa sinema, au pia uchezaji*
*Wa kipaji husimama, kipaji kina mtaji*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***MAZINGIRA***

*Leo ninayo hasira, natetea mazingira*
*Mbona mwaleta hasara, mazingira kuyazira*
*Ebu nawapa busara, yatunzeni mazingira*
*Mazingira mazingira! Tuyatunze mazingira*

*Tuyatunze mazingira, kichwa tuache kufura*
*Mvua ikishatugura, wataenda wapi chura?*
*Misitu yenye sungura, 'meharibu wazurura*

*Mazingira mazingira! Tuyatunzeni daima.*

*Tuyatunzeni daima, kwa bidii na akili*
*Miti imejaa dhima, nyingi siwezi nakili*
*Kama nyumba za wanyama, na hutibu pia mwili*
*Mazingira mazingira! Yatupasa kuyatunza.*

*Yatupasa kuyatunza, faida zake ni nyingi*
*Moja moja kujifunza, ni muhimu siwapingi*
*Ewa safi ni ya kwanza, kupunguza joto jingi*
*Mazingira mazingira! Humo ndimo tunaishi*

*Humo ndimo tunaishi, bora tuyaweke safi*
*Magonjwa yenye ubishi, yatoke tuwe hatufi*
*Kipundipindu tapishi, huchafua hadi Sufi*
*Mazingira mazingira! Takataka tuokote*

*Takataka tuokote, Shuleni hadi nyumbani*
*Tuwe safi kotekote, Sio nje sio ndani*
*Maji taka siyachote, wala situpe mitoni*
*Mazingira mazingira! Usafi penda kuganda.*

*Usafi penda kuganda, kwa majumba na vibanda*
*Uchafu kwenye viwanda, usalama wake kupanda*
*Majini usije ganda, samaki wakala sanda*
*Mazingira mazingira! Magari sitoe moshi.*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***WALEMAVU***

*Walemavu tuwapende, mbali nao tusiende*
*Mambo mema tuwatende, tuwatunze kila pande*
*Kwa upendo tuwagande, Furaha kwao itande*
*Walemavu wana haki, Pia wao binadamu.*

*Kwa Hakika wanaweza, wana nguvu bila shaka*
*Ni vibaya kuwabeza, tuwape wanachotaka*

*Kazi njema wanakweza, nafasini kiwaweka*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu.*

*Wana nguvu maalumu, wanao tele uwezo*
*Waishikapo hatamu, wanafanya si mchezo*
*Jamani tuwape zamu, waongoze bila bezo*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu.*

*Tusiwabague katu, tuwapatie usawa*
*Japo kushona kiatu, wanaweza wakipewa*
*Tuwaone kama watu, si kinyama kukemewa*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu.*

*Tujitahidi wasome, kwenye shule maalumu*
*Ujinga kwao ukome, wajawe utaalamu*
*Pongezi kwao zivume, mazuri wayafahamu*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu.*

*Tamaduni zilo duni, tuzionyeshe kisogo*
*Tuzichome kama kuni, wakubwa na kwa wadogo*
*Walemavu si kunguni, tusiwapatie pigo*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu.*

*Vyovyote tunavyoweza, tuwasaidie jama*
*Mazuri wanayoweza, nafasi tuwape hima*
*Na pale wasipoweza, pamoja nao simama*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu.*

*Haki zao na tuwape, chochote tusiwanyime*
*Viboko tusiwachape, daima tuwape shime*
*Kuwatunza na tuape, Pamwe nao tusimame*
*Walemavu wana haki, pia wao binadamu*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***NAMLA SAMAKI***

*Nasema wangu Samaki, namla*
*Kabisa kwangu habaki, namla*
*Kwa sana bila hamaki, namla*

*Njaa ikinishitaki, namla*
*Bila Samaki sitaki, namla.*

*Namla, Samaki wa bei ghali*
*Namla, Samaki kwao ugali*
*Namla, Miiba yake sijali*
*Namla, kinidunga ni ajali*
*Namla, tamu yake ya asali.*

*Nimekesha kwa bahari, namla*
*Mvuvi Nina fahari, namla*
*Hadi mwisho wa dahari, namla*
*Kumpika ni hodari, namla*
*Tamu yake ni johari, namla*

*Namla, Samaki huyo ni kazi*
*Namla, Malipo yake ni ngazi*
*Namla, Biashara ndo jahazi*
*Namla, hata iwe kiangazi*
*Namla, tamu yake iko wazi.*

*Kazini metoa jasho, namla*
*Nimesoma kwa kopesho, namla*
*Samaki aso na mwisho, namla*
*Ni Elimu ya somesho, namla*
*Tamu yake bila bishop, namla*

*Namla, Samaki wangu kipaji*
*Namla, daima nipate taji*
*Namla, namuweka kwenye maji*
*Namla, niyakidhi mahitaji*
*Namla, tamu yake ni siraji.*

*Samaki wa ukarimu, namla*
*'Tajikaza nihitimu, namla*
*Kuwafaa wenye hamu, namla*
*Mazuri kila sehemu, namla*
*Walemavu wone tamu, namla*

*Namla, samaki msaidizi*
*Namla, kuifukuza ajizi*
*Namla, wengine kuwapa ngazi*
*Namla, nifae waso mavazi*
*Namla, tamu yake ni andazi.*

*Samaki wa darasani, namla*
*Katu wasiwe gizani, namla*
*Ujinga siambizani, namla*
*Kufunza walo gizani, namla*
*Tamu yake vitabuni, namla.*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***USILAZE YAKO DAMU***

*Chonde Chonde wanafunzi, tegeni lenu sikio*
*Nawawashia kurunzi, mpate mafanikio*
*Leo nawapa utunzi, Sikia kiitikio*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

*Masomoni tia nguvu, Usome tena kwa nia*
*Wala sio kwa mabavu, ila akili tumia*
*Daima tikisa wavu, wa masomo mia mia*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

*Hakuna alotimia, pungufu pia hakuna*
*Mungu kakukirimia, uwezo ebu kazana*
*Kipaji ukitumia, Mengi mema utavuna*
*Jikaze ufanye mema, usilaze yako damu.*

*Jitahidi Hisabati, kimombo na kiswahili*
*Sayansi ikarabati, Somo la dini himili*
*Masomo kila wakati, jikaze kwa kila haki*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

*Masomo hayana mwisho, Popote pale jifunze*
*Usiogope vitisho, Akili yako itunze*
*Sihofu kutoa jasho, umilisi kajifunze*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

*Siishie darasani, jifunze hadi shambani*
*Sio tu ukurasani, Jifunze na ya jikoni*
*Jifunze hadi hisani, na kuishi maishani*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

*Kajifunze kujifunza, mwenyewe kwa taratibu*
*Kwenye mitandao kwanza, kalisakure jawabu*
*Lolote likikutanza, tekinolojia jibu*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

*Usilaze yako damu, katafute umilisi*
*Jifunze utaalamu, huletao ufanisi*
*Sio tu kazi kalamu, Bali kazi za halisi*
*Jikaze ufanye vyema, usilaze yako damu.*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***<u>HESHIMA</u>***

*Heshima jama heshima, ipande na isishuke*
*Heshima ndio hekima, sikubali ikuruke*
*Heshima huleta mema, Popote pale uvuke*
*Heshima yako dumisha!*

*Heshima yako dumisha, Popote ikuongoze*
*Heshima inavumisha, kokote wakupongeze*
*Heshima yanawirisha, yoyote ikuongeze*
*Heshima yako zidisha!*

*Heshima yako zidisha, kwa ndugu na majirani*
*Heshima yenye kupisha, wakongwe wako njiani*
*Heshima ya kuvukisha, Vipofu barabarani*
*Heshima yako idumu!*

*Heshima yako idumu, kwa wakubwa na wadogo*

*Heshima kwenye salamu, kwa wote hadi wadogo*
*Heshima sio sanamu, watu kuwapa kisogo*
*Heshima yako itunze!*

*Heshima yako itunze, popote iwe lazima*
*Heshima tele jifunze, adabu kutoizima*
*Heshima usiikinze, fanya mambo kwa kupima*
*Heshima yako thamani!*

*Heshima yako thamani, kazini na kwa jirani*
*Heshima si uzamani, wengine wanatamani*
*Heshima kama samani, ni pambo hadi kortini*
*Heshima ni masomoni!*

*Heshima ni masomoni, Mengi mema hutujuza*
*Heshima jaa pomoni, tufae hadi ajuza*
*Heshima ya midomoni, matusi kutosambaza*
*Heshima yako hekima!*

***Duncan Mulu (Malenga wa LungaLunga)***

## ***LISOME SHAIRI LOTE***

*Lisome shairi lote, 'nzia mwanzo hadi mwisho,*
*Twasira ukaipate, isiyokuwa na jasho,*
*Ma'na ya umbo upate, bila yoyote matisho,*
*Ino hatua ya kwanza, wangwana ninawajuza.*

*Tena kusoma rudia, lakini kwa pole pole,*
*Kurudia tasadia, upate maana tele,*
*M'ana hiyo andikia, weze lewa polepole,*
*Ino hatua ya pili, wasomi ninawambia.*

*Lisome tena shairi, mshororo moja moja,*
*Lisome kwa tafakari, kwa makini ya pamoja,*
*Yapigie mstari, kwako isiwe kioja,*
*Ino hatua ya tatu, wenzangu mzingatie.*

*Kwa undani tafakari, ulopiga mistari,*
*Maana ya ushairi, kwa kweli itadhihiri,*

*Sipoelewa vizuri, lissome tena shairi,*
*Ino hatua ya nne, wadau ninawasihi.*

*Vipengele vya sanaa, vichunguze kwa makini,*
*Utakuja kugundua, vipi kuingiliani,*
*Tafakari yaweza kua, hata piya na mizani,*
*Ino hatua ya tano, wapenzi namfahamu.*

*Pamoja wewe ziweke, hizo zako fafanuzi,*
*Maana fungamanike, ushairi uwe wazi,*
*Wako 'shahidi uweke, maana uje maizi,*
*Ino hatua ya sita, pia ni vyema kujua*

*Ule mtazamo wake, mtunzi ukaonyeshe,*
*Dhamira hiyo ya kwake, mwenzangu ujijulishe,*
*Dhamira hiyo ya kwake, maudhui ikupeshe,*
*Ino hatua ya saba. Isije sahaulika.*

*Hatua namalizia, vyema nimeelezea,*
*Tungo kutathiminia, Mshairi kulezea,*
*Uzuri wake onyeshea, hata udhaifu pia,*
*Ino hatua ya nane, ambayo ndio ya mwisho.*

***Vincent Okwetso (Malenga Mkomavu)***

## ***TUNGO ZA LADHA***

*Tunga ndugu tunga tungo, tungo zilo na ubora,*
*Tunga usone mapingo, mapingo yaso kukera,*
*Tunga kwa chako kiwango, kiwango sicho uchwara,*
*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

*Tunga mwenzangu utunge, utunge bila kuchoka,*
*Tunga uweze jiunge, jiunge na wasifika,*
*Tunga usijejitenge, usijitenge hakika,*
*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

*Tunga wewe ukiwaza, ukiwaza kwa makini,*
*Tunga hata ukicheza, ukicheza uwanjani,*
*Tunga lugha kutukuza, kutukuza kwa maoni,*

*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

*Tunga hata beti mbili, mbili beti za ubora,*
*Tunga ukijisaili, ukisaili fikira,*
*Tunga ukifikili, kifikili ya ubora,*
*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

*Tunga wewe ukijua, ukijua ya kutunga,*
*Tunga hata kwa Jalia, Jalia wa kutujenga,*
*Tunga ukimsifia, kimsifia kwa kinga,*
*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

*Tunga ukizifutia, kizifuatia arudhi,*
*Tunga vina kiwekea, ukiwekea kwa ridhi,*
*Tunga pasi kukosea, kukosea ya arudhi,*
*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

*Tunga utungo wa kweli, kweli tungo namaliza,*
*Tunga wewe ukijali, ukijali naeleza,*
*Tunga tungo za asali, asali ya kulambiza,*
*Watunzi tutunge tungo, tungo zilizo na ladha.*

***Vincent Okwetso (Malenga Mkomavu)***

## ***UKIPATA WA KUPENDA***

*Ukipata wa kupenda, hakika wewe mpende,*
*Usije ukamtenda, na zako ukaziende,*
*Jukumlo kumulinda, hata akiwa hawinde,*
*Ukipata wa kupenda, hakika wewe mpende.*

*Ukipata wa kupenda, mshukru mola wako,*
*Usiwache akakonda, kama yeye sio wako,*
*Asije patwa na donda, ajili iwe ya kwako,*
*Ukipata wa kupenda, hakika wewe mpende.*

*Ukipata wa kupenda, mtunze wewe mwenzangu,*
*Kwako yeye ni ja chanda, yasimpate machungu,*
*Mtunze wa kwako nyonda, yasimtande mawingu,*
*Ukipata wa kupenda, hakika wewe mpende.*

*Ukipata wa kupenda, muonyeshe lako penzi,*
*Piya uweze mfunda, agundue lako penzi,*
*Sisahau kumkanda, uyaondoe majonzi,*
*Ukipata wa kupenda, hakika wewe mpende.*

*Ukipata wa kupenda, Kaditama nimefika,*
*Kwako yeye ataganda, hataondoka hakika,*
*Kwake ukuwe muunda, kwake iwe mtajika,*
*Ukipata wa kupenda, hakika wewe mpende.*

***Vincent Okwetso (Malenga Mkomavu)***

***KISWAHILI KITUKUZWE****.*

*Ya mgambo imelia, jueni kunalo jambo,*
*Ningependa kuwambia, mengi mfahamu mambo,*
*Jambo hili mewazia, tangu enzi za kitambo,*
*Kitukuzwe Kiswahili, duniani kisikike.*

*Hebu tegeni sikiyo, vyema muweze sikiza,*
*Nawapea mgogoyo, Kiswahili kukikuza,*
*Waandishi si wachoyo, lugha ino wanakuza,*
*Kitukuzwe Kiswahili, duniani kisikike.*

*Kinasemwa Kiswahili, kila pembe ya dunia,*
*Twakipenda ja asali, kwa wingi kukitumia,*
*Hata ndani kwenye meli, wasafiri hutumia,*
*Kitukuzwe Kiswahili, duniani kisikike.*

*Mahakama ukienda, lugha yao Kiswahili,*
*Ino ishara kupenda, lugha iliyo aali,*
*Tujitolee kulinda, chetu kino Kiswahili,*
*Kitukuzwe Kiswahili, duniani kisikike.*

*Natamatisha nudhumu, tano beti zimebisha,*
*Ujumbe na mfahamu, Kiswahili kinalisha,*
*Ni letu sote jukumu, lugha ino kuboresha,*
*Kitukuzwe Kiswahili, duniani kisikike.*

***Vincent Okwetso (Malenga Mkomavu)***

***KAZI KUBWA NI KULEA.***

*Naandika kueleza, yale yalio muhimu,*
*Nye wazazi kuwajuza, mambo yaliyo matamu,*
*Vibaya sije kuwaza, mkaanza nishutumu,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Mwana ukisha mzaa, ni mengi mahitaji,*
*Kheri hili kulijua, mweze jua mahitaji,*
*Mbele mwaweza jutia, kujifanys wajuaji,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Chakula chahitajika, siha aipate mwana,*
*Afya sije zoroteka, ghulamu kwa msichana,*
*Mzazi utasifika, hadi uitwe jagina,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Yahitajika mavazi, mwili mwana avalie,*
*Sasa huu ni ulezi, wako mwana furahie,*
*Wahitajika ujuzi, hili lije kutimie,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Elimu ni yake haki, mwana aweze ipata,*
*Mbele asipate dhiki, dhiki iliyo matata,*
*Ujuzi aje miliki, pasi na kwona utata,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Tabia njema zafaa, kuwa nayo wako mwana,*
*Asije kutabikia, yeye napochangamana,*
*Mwishowe aje jutia, kulaumu wake nina,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Kazi zilo za nyumbani, ni vyema mwana kufunzwa,*
*Asifike ukubwani, hakuna alichofunzwa,*
*Ajipate matatani, vibaya kiwa kutunzwa,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Kama wewe ni mzazi, mwana simunyime pendo,*

*Huu piya ni ulezi, ule wa bora matendo,*
*Tapenda wako uzazi, uzazi wenye mapendo,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Katika huko kulea, msiwe wa kubagua,*
*Jinsia kupendelea, wa kiume kutesea,*
*Mwana aje tesekea, kusudi kupendelea,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

*Ashara zimetimia, beti zangu nazifunga,*
*Wazazi nawasihia, wana wenu kuwakinga,*
*Mwana wote kuwalea, ni vyema weze jipanga,*
*Kuzaa mwana si kazi, kazi kubwa ni kulea.*

***Vincent Okwetso (Malenga Mkomavu)***

***AMANI NI TUNU***

*Okwetso ninaandika, amani kiangazia,*
*Ni heri tukikumbuka, amani kuikuzia,*
*Naeleza kwa hakika, nasi tuje kuridhia,*
*Amani kwetu ni tunu, ni tunu yenye thamani.*

*Wakenya tukikumbuka, mwaka elfeni saba,*
*Amani ilitoweka, vurugu ikatukaba,*
*Amani livurugika, vita vikawa ni baba,*
*Amani kwetu ni tunu, ni tunu yenye thamani.*

*Ama vipi mnataka, iweze kukuwa hali?*
*Heri natujue fika, amani kitu aali,*
*Vema mambo keleweka, hali itakuwa tuli,*
*Amani kwetu ni tunu, ni tunu yenye thamani.*

*Wakenya kiaminika, kwamba amani ni tunu,*
*Sote tutabidiika, tusivipasuwe vinu,*
*Amani ikisifika, taiona yake tunu,*
*Amani kwetu ni tunu, ni tunu yenye thamani.*

*Tusiwe wa kuokoka, pasi kukuza amani,*
*Takuwa kudanganyika, na kujipata shimoni,*

*Hali ikilainika, itajengeka amani,*
*Amani kwetu ni tunu, ni tunu yenye thamani.*

*Okwetso mwisho nafika, kauli nikiifunga,*
*Ni bora tukikumbuka, amani kwetu ni mwanga,*
*Tusipende kupofuka, bila amani kujenga,*
*Amani kwetu ni tunu, ni tunu yenye thamani.*

***Vincent Okwetso (Malenga Mkomavu)***

***MAISHA***
*Ya hapa kwetu maisha, hayaishiki,*
*Chakula ukujilisha, hakilikiki,*
*Bei wameipandisha, haishukiki.*

*Dukani kukinunua, hakinunuki,*
*Gharama wameinua, haishukiki,*
*Kwa ushuru kwongezea, haupunguki.*

*Kijaribu kulalama, hausikiki,*
*Na huko kurudi nyuma, hakurudiki,*
*Maneno wanayosema, siyaridhiki.*

*Gesi pia imepanda, haijaziki,*
*Moshi wa kuni mkosi, huvumiliki,*
*Ni heri kuwa farasi, hausumbuki.*

***Allan Lumanyasi Chevukwavi (Mwoshashombo)***

***SITISHIKI***
*Nakuita, huitiki, wanirushia matusi,*
*Nakupita, hupitiki, unanipiga mkasi,*
*Wanikata, sikatiki, unamelewa chunusi.*

*Waninyonga, sinyongeki, unapata wasiwasi,*
*Wanipinga, sipingiki, nasonga mbele kwa kasi,*
*Wanichenga, sichengeki, washindwa kupiga pasi.*

*Wanipiga, sipigiki, nakimbia na farasi,*

*Wanitega, sitegeki, nina wengi majasusi,*
*Waniroga, sirogeki, wakula mwenyewe nyasi.*

***Allan Lumanyasi Chevukwavi (Mwoshashombo)***

***UTU***

*Sipigani, kutetea kiso changu,*
*Sipigani, kuushinda ulimwengu,*
*Sipigani, waje kunitia pingu,*
*Napigana, kujenga dunia njema.*

*Sishukuru, kwa kupata kila kitu,*
*Sishukuru, kwa kumiliki msitu,*
*Sishukuru, nikiona wenye kutu,*
*Nashukuru, kwa wanitendao utu.*

*Sipongezi, wajijazao matumbo,*
*Sipongezi, wapiga wenzi makumbo,*
*Sipongezi, wapendao majigambo,*
*Napongeza, wagawanao makombo.*

*Sitauma, wale wa kutenda mema,*
*Sitauma, watoa kwa kujinyima,*
*Sitauma, wamaliza ulitima,*
*Nitauma, wenye kupenda khasama.*

*Sitanyonga, wananchi wazalendo,*
*Sitanyonga, waendezao upendo,*
*Sitanyonga, wa miema mienendo,*
*Nitanyonga, wote wanuka uvundo.*

*Sikemei, wainuao uchumi,*
*Sikemei, na kweli wanojihami,*
*Sikemei, wajenga njia za lami,*
*Nakemea, wakutudhuru watemi.*

**MWANA JIKAZE**

Jikaze mwana jikaze,dunia haina rahisi
Inuka damu silaze,kazi ikupe libasi
Nitakuchezea zeze,na nyimbo zisizo hasi
Hewala jasho litoze,usife kwa kuwa bosi

Tafuta fulusi mwana,tafuta hata mkopo
Kopa hata na matwana,ulipe kwa pole hapo
Pikipiki pia ona,malipo ya pole yapo
Hapa jingine sina,wasia ndio ulipo

Tafuta mkunde mwana,chuuza barabarani
Ufyefye mwana hapana,jitoe jitie kazini
Duniya raha haina,hukata wazembe ini
Mla leo ndiwe mwana,na mla Kesho kalani

Beba maji sana sana,yauze hasa mijini
Usione haya mwana,hata ukiuza kuni
Binadamu hujikuna,ionapo yake mboni
Hiyo ndo yangu amana,ya wosia maishani

Yarabina akulinde,mwanangu ushike yangu
Kesho nikienda nende, nawe wepuke machungu
Ya ziraili ushinde,mbawazi akupe Mungu
Kumbuka duniya pinde,jikaze sana mwanangu
Wadi sandichi.

**-Wadi Sandichi**